# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Tano – Tarehe 19 Septemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Maelezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 *[Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004]*.

**MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 *[Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004]*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhan Ighondo, kwa niaba ya Mwenyekiti.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWEYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 68

**Madereva wa Mabasi ya Abiria na Mizigo Kupewa Mikataba**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kuhakikisha Madereva wa magari ya abiria na mizigo wanapewa mikataba ya kazi ili kupata mafao na Bima za Afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kusimamia Sheria za Kazi na kuwahimiza waajiri wote nchini kuwapatia wafanyakazi wao mikataba ya ajira kwa kuwa hili ni takwa la kisheria na ni haki ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhimza hili Serikali ilitoa tamko na maagizo kwa wamiliki wa mabasi na malori tarehe 12 Juni, 2022 na tarehe 22 Julai, 2022, kwamba ifikapo tarehe 30 Agosti, 2022, wafanyakazi madereva wote wawe wamepewa mikataba kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa waajiri wengi wametekeleza na baadhi bado wanaendelea kutekeleza mikataba hiyo kwa ajili ya kuwapatia madereva, lakini pia wafanyakazi wote katika sekta rasmi nchini. Aidha, Ofisi imejipanga na inaendelea kufanya

ukaguzi maalum katika Sekta ya Usafirishaji na kuchukua hatua stahiki kwa waajiri wanao kiuka takwa hilo la kutoa mikataba kwa wafanyakazi madereva na Sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua na kulinda haki za wafanyakazi madereva, imeweka utaratibu wa kukaa Vikao vya Mashauriano na Majadiliano na Viongozi wa Vyama vya Wamiliki wa Vyombo vya Usafirishaji (Malori na Mabasi) pamoja na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi Madereva kwa lengo la kupeana taarifa kuhusu changamoto zinazowakabili madereva na kuzitafutia ufumbuzi. Aidha, utaratibu huu ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti mbali na kaguzi hizo, nitoe rai na kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kutoa taarifa endapo watapata taarifa za kutokuwepo kwa mwajiri katika sekta hii ambaye bado hajatekeleza maagizo haya ya Serikali kwa kutoa mikataba ya ajira kwa wafanyakazi madereva, hatua stahiki zitaendelea kuchukuliwa pia kwa mujibu wa sheria kwa kutambua kwamba sekta hii ni muhimu na ina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu.  Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa madereva wengi wamekuwa wakifanya kazi na kupata ajali lakini na matatizo mengine ya kiafya hali ambayo wanakuwa mzigo kwa familia. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia hawa madereva waweze kupata haki zao za msingi kuepukana na vifo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tamko limetolewa muda mrefu na mpaka sasa kuna baadhi ya wamiliki wa magari hayo hawajatoa mikataba hiyo. Je, nini tamko la Serikali kuhusiana na hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, madereva ambao wanaopata ajali au maafa kutokana na kazi ambazo wanazifanya, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)* ambao unawajibika na kuhakikisha kwanza maeneo yote rasmi ya waajiri yanasajiliwa na kutoa michango kwa ajili ya fidia pale mfanyakazi anapopata madhila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo Sheria ya *Workers Compensation* ambayo nayo pia inahusika na masuala ya ulipaji fidia. Sambamba na hilo Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, amefanya mabadiliko na maboresho kwenye sheria za bima ambapo vyombo hivi vinakatiwa bima na zipo bima ambazo zinawa-*cover* pia wale ambao watapata madhila kutokana na ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Kisangi ameuliza kuhusu waajiri ambao hawajatoa mikataba. Naomba nitoe tamko rasmi la Serikali kama jinsi alivyonitaka nifanye, tamko rasmi ni kwamba, ni kosa kisheria kama umeajiri mfanyakazi na haumpatii mkataba, kwa sababu sheria zinatoa maelekezo, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, inatoa haki za mfanyakazi, lakini pia wajibu wa mwajiri. Wajibu wa mwajiri unaelezwa katika sheria hiyo zikiwa ndiyo haki za mfanyakazi. Kwa hiyo, ina *reciprocate* kwamba haki za mwajiri, ndio wajibu wa mfanyakazi na wajibu wa mfanyakazi ndio haki za mwajiri. Kwa hiyo, mtu yoyote ambaye hatatoa mkataba wa kazi na maeneo hayo tumekuwa tukiyabaini, tumekuwa tukiwachukulia hatua na ikibidi kuwapeleka mahakamani ili waweze kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa maeneo yote Watanzania wanaonisikiliza lakini pia Waheshimiwa Wabunge, kama kuna maeneo ambayo tuna uhakika kwamba hawatoi mikataba ya kazi pamoja na kaguzi zetu mtupe taarifa ili tukachukue hatua stahiki kwa wakati unaostahili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Patrobas Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini aulize swali lake.

Na. 69

**Fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Vituo vya Afya Ukata na Litumbandyosi – Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Ukata na Litumbandyosi, Halmashauri ya Wilaya Mbinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilipeleka Shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi Kituo cha Afya cha Kimkakati katika Kata ya Mkumbi iliyopo Tarafa ya Mkumbi. Kituo hiki cha kimkakati kitahudumia Kata sita (6) za tarafa hiyo ikiwemo Kata ya Ukata. Ujenzi wa Kituo hicho cha Afya upo katika hatua za umaliziaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga katika mwaka 2022/2023, imetenga Shilingi milioni 500 fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Litumbandyosi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa majibu hayo lakini nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba vituo hivi vya kimkakati tulikubaliana, pamoja na kujengwa Makao Makuu ya Kata, lakini pia vijengwe kwenye kata zile za mbali. Kwa hiyo, Kata ya Ukata iko mbali sana na hiki kituo cha Mkumbi. Kwa hiyo, nini maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali ilipeleka fedha milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mapela na mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya vifaa tiba Shilingi milioni 320, lakini mpaka leo hii vifaa tiba katika kituo hiki cha afya havijafika. Sasa nataka kujua fedha hizi ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kituo hiki cha Mkundi, Matiri, pamoja na Muungano, sasa hivi vimeshakamilika. Ni lini sasa tutapeleka watumishi pale ili vianze kufanya kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilitoa mwongozo wa kujenga vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati, vigezo vikiwa kwanza idadi ya wananchi katika eneo husika, lakini pili, umbali wa kituo kile kutoka kituo cha karibu zaidi au hospitali ya karibu zaidi. Kwa hiyo, ukitoa kata yoyote ambayo inakidhi vigezo hivyo ina sifa ya kuwa kata ya kimkakati kwa ajili ya kituo cha afya. Kwa taarifa tulizonazo bado idadi ya watu sio kubwa sana, kwa hivyo inakosa ile sifa kuwa kituo cha afya cha kimkakati kwa maana ya idadi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 400 zilipelekwa katika kituo cha afya alichokitaja Mheshimiwa Mbunge na milioni 320 za vifaa tiba tayari zimepelekwa Bohari Kuu ya Madawa *(MSD)* kwa ajili ya kuleta vifaa hivyo. Tunaendelea kushikirikiana na Wizara ya Afya, kuhakikisha vifaa hivyo vinaletwa mapema iwezekanavyo ili huduma za afya zianze kutolewa katika kituo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hivi vituo vitatu vilivyokamilika, kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha nyingi kukamilisha vituo vya afya vitatu na nimhakikishie Mbunge kwamba mpango wa ajira kwa watumishi kwa awamu ni kuhakikisha kwamba tunaleta watumishi kwenye vituo hivyo pia ili huduma zianze kutolewa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Manufaa ya kuunganisha Idara ya Kilimo katika Halmashauri**

**MHE YUSTINA A. RAHHI** aliuliza:

Je, kuna manufaa gani ya kuunganisha Idara ya Kilimo na Mifugo katika Halmashauri za Wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekit, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa uandaaji wa muundo na mgawanyo wa majukumu huzingatia mambo mbalimbali ikiwemo Sera, Sheria na maelekezo ya Serikali ya wakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Halmashauri za Wilaya uliidhinishwa rasmi tarehe 29 Januari, 2022, baada ya kufanya mapitio kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Katika mabadiliko hayo, Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika na Idara ya Mifugo na Uvuvi iliunganishwa na kuwa Idara moja ya Kilimo na Mifugo kutokana na kushabihiana kwa majukumu ya Idara ya Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa ya kuhuisha miundo katika ngazi ya halmashauri na Mikoa ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu, kupunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha uratibu na usimamizi. Hivyo, muundo mpya wa halmashauri umepungua kutoka Idara 13 na Vitengo Sita na kuwa na Idara Tisa na Vitengo Tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Taasisi hizo unaweza kufanyiwa mabadiliko inapohitajika bila kuathiri ufanisi ili kukidhi utendaji kazi wa kila siku. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa katika ngazi ya Wizara, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni Wizara mbili tofauti zenye majukumu tofauti. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ndiyo Wizara zilizopewa fedha nyingi za miradi, watendaji wa Wizara hizi wako katika halmashauri. Je, sasa kwa mfano Wizara moja inapotoa maelekezo halmashauri na kwenda kusimamiwa na mkuu wa idara nyingine, mfano Wizara ya Kilimo, kutoa maelekezo kwa Mkuu wa Idara ya Mifugo, je, hakutarudisha ufanisi wa utendaji wa kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Idara hizi za Kilimo na Mifugo katika halmashauri ndizo zinazotegemewa kwa mapato ya ndani, sasa kumwachia majukumu mkuu wa idara moja kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kilimo, mifugo na uvuvi, je, hakutaathiri ukusanyaji wa mapato katika halmashauri hizo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo ni Wizara mbili tofauti kwa ngazi ya Wizara, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara zikiwa tofauti haimaanishi kwamba *coordination* ya kuwatumia na kuwaelekeza Wakuu Idara katika Halmashauri inakwama. Halmashauri zetu zinatofautiana, kuna halmashauri ambazo zinashughuli nyingi zaidi za mifugo, kuna halmashauri nyingi zaidi ambazo ni za kilimo. Wakuu wa Idara wa Halmashauri hizo itazingatiwa halmashauri ina idadi kubwa zaidi ya shughuli gani, kama ni za kilimo, Mkuu wa Idara atakuwa ni Afisa wa Kilimo. Kama ni mifugo Mkuu wa Idara atakuwa ni mtaalam wa masuala ya mifugo na *coordination* ya Serikali ni moja mpaka chini bila kujali utofauti wa Wizara katika ngazi ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mapato ambayo yanakusanywa kutoka Idara ya Kilimo na Idara ya Mifugo, ikumbukwe kwamba wataalam wote wa mifugo wanaendelea kuwepo na Wakuu wa Idara kwa maana ya wataalam wetu wa kilimo wanaendelea kuwepo, kinachotofautisha ni mkuu wa idara lakini ataendelea kuwaratibu na kuwasimamia wataalam katika ukusanyaji mapato katika kusimamia shughuli za kilimo na mifugo kwa muktadha huo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Malipo kwa Watumishi waliohamishiwa Halmashauri ya Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:

Je, ni lini Serikali itawalipa Watumishi waliohamishiwa katika Halmashauri ya Chemba?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilianzishwa rasmi tarehe Mosi Julai, 2013, baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kugawanywa. Jumla ya watumishi 90 wa idara mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, walihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ambao walistahili kulipwa kiasi cha Shilingi milioni 238.7 ikiwa ni stahiki zao za kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilihakiki madeni ya watumishi hao na kuwasilisha Serikali Kuu maombi ya kulipwa madeni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba katika mwaka wa fedha 2023/2024, itatenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kulipa madeni hayo. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti za kila mwaka ili kuendelea kulipa madeni hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nasikitika kidogo kwa majibu ambayo Serikali imetoa, anakubaliana kwamba uhakiki umekamilika tangu 2015 na sasa ni miaka nane mpaka leo watumishi wale hawajalipwa hata shilingi moja. Hata hivyo, kinachosikitisha zaidi, wapo waliostaafu lakini pia wapo ambao wamekufa. Nataka kujua nini hatima ya hao waliostaafu na hao waliokufa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulipa madai yoyote ya watumishi lazima uhakiki kujiridhisha zaidi ya shaka kwamba wanaodai wanadai kiwango halali na wanastahili kulipwa malipo hayo. Ni kweli kwamba uhakiki ulianza mwaka 2015/2016, lakini kuna dosari nyingi za madai zilionekana miongoni mwa wale ambao walitakiwa kulipwa na Serikali isingeweza kuwalipa kabla ya kujiridhisha kwamba kiasi ambacho wanadai wanatakiwa kulipwa. Kwa hiyo, baada ya Mkaguzi wa Ndani kutoka Makao Makuu kufanya ukaguzi, ikaonekana madai yale yameshuka na ndiyo maana yamechelewa kuanza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka ujao inatengwa fedha, lakini kila mwaka tutatenga fedha kuhakikisha wote waliostaafu, walioko kazini na hata ambao wametangulia mbele za haki wanalipwa kwa kupitia wale ndugu ambao ni wategemezi wa hao waliotangulia mbele za haki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 72

**Mradi wa Maji - Vuga – Mlembule - Mombo – Korogwe**

**MHE. MWANTUM M. ZODO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa Vuga - Mlembule katika Mji Mdogo wa Mombo Wilayani Korogwe?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Maryprisca.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Mzamilu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa Vuga - Mlembule ulioanza kutekelezwa mwezi Julai, 2020 ambapo utekelezaji hadi sasa umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2022. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)*, ujenzi wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 500, ujenzi wa matanki punguza mawili (2) na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa Kilometa 10.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazoendelea ni ujenzi wa matanki punguza manne (4) na ulazaji wa mabomba ya usambazaji Kilometa 4.3. Kukamilika kwa mradi huu kutanufaisha wananchi wapatao 21,284 wa Vijiji vya Mlembule, Mwisho wa Shamba, Mombo na Jitengeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUM M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Mkomazi na Kata ya Mkalamo katika Jimbo la Korogwe Vijijini ni Kata ambazo zimepitiwa na Mto Ruvu lakini Kata hizo hazina maji kabisa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanapeleka maji kwenye Kata hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mradi mkubwa wa maji wa Mwanga, Same, Korogwe ni mradi ambao unasuasua. Je, Serikali ina mpango gani wa kwenda kukamilisha mradi huo wa maji ili kuondoa adha ya maji kwa wananchi wa Wilaya ya Korogwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zodo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Zodo kwa ufuatiliaji mzuri kwani wakinamama lazima tusemeane na tuhakikishe tunawatua ndoo kichwani akinamama wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hizi mbili alizoziongelea za Korogwe Vijijini zipo kwenye mpango, mradi huu ukishakamilika kwa awamu hii ambayo utekelezaji unaendelea awamu inayofuata Kata hizi Mbili pia zitapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mradi wa Mwanga, Same, Korogwe nimetoka huko hivi majuzi mradi ni mzuri sana na kazi zinaendelea. Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka kwenye maeneo ya mradi huu baadhi tuliweza kuongozana mradi ni wa mafanikio makubwa sana na unaendelea kutekelezwa na utakuwa manufaa maeneo yote ambayo unapitia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Zodo. Tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde sasa aulize swali lake.

Na. 73

**Kuongeza Wigo wa Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wigo wa biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ili kuongeza mapato?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina Mipango na Mikakati mbalimbali ili kuendelea kupanua wigo wa Biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar ikiwemo:

(i) Kuendelea kutoa elimu na kuongeza hamasa zaidi kwa makampuni ya Tanzania Bara na Zanzibar kushiriki katika Maonesho mbalimbali yanayofanyika ndani ya Tanzania Bara na Zanzibar;

(ii) Kufanya tathmini na kubaini vizuizi visivyo vya kikodi;

(iii) Kuzishirikisha Mamlaka mbalimbali ikiwemo Mamlaka za Mapato za Tanzania Bara *(TRA)* na Zanzibar *(ZRA)* kwenye majadiliano ya pamoja ili kupanua wigo wa Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upanuzi wa ushirikiano wa kibiashara unazingatia na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyonipatia kwenye swali langu hili la msingi, maswali yangu ni kama ifuatavyo.

Kwa vile amesema kwamba Serikali ina mpango wa kuondosha vizuizi vya biashara. Je, Serikali ina mpango gani wa kuviunganisha vyombo ambavyo vinazuia biashara kuwa na kasi kwa mfano, *ZBS* na *TBS* kuweza kuunganika na ikiwa mzigo umekaguliwa Zanzibar iwe imetosha ama mzigo ikiwa umekaguliwa Tanzania Bara iwe imetosha. *(Makofi)*

Swali la pili, kwa vile tunataka kuongeza mapato ya wananchi pamoja na Serikali; Je, sasa Wizara yako haioni ni wakati wa kukaa na Wizara ya Fedha ili kuiruhusu biashara kufanyika wakati wa siku za Jumapili kama zilivyo *border* nyingine ambazo zinafanyakazi siku Saba kwa wiki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Said Issa Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli moja ya mikakati ambayo tunaiweka ni kuona namna gani tutaboresha kwa kuunganisha baadhi ya taasisi ambazo zinafanyakazi zinazofanana kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ikiwemo hizi za *ZBS* na *TBS*. Lakini kwa sababu haya ni mambo ya Kimuungano naomba tuendelee kuyafanyia kazi ili tuweze kuona namna gani tutaendeleza mashirikiano kati ya mamlaka hizi mbili na mamlaka nyingine ambazo zinashirikiana katika kufanyakazi zinazofanana kati ya pande hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kweli moja ya vitu ambavyo tunavifanya katika kuhakikisha tunaongeza mapato ni kuboresha au kurahisisha ufanyaji biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara tunachukua ushauri huu ili tuweze kuona namna ya kukaa na wenzetu Wizara ya Fedha na Mipango kuboresha siku ambazo ni za sikukuu au Jumapili au *weekend* ambazo wakati mwingine kunakuwa na changamoto ya ufanyajikazi ili tuweze kuwahudumia wafanyabiashara vizuri waweze kufanya shughuli zao katika siku hizi za *weekend*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe. Tunaendelea na Wizara Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Amour Hamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, sasa aulize swali lake.

Na. 74

**Idadi ya Wavumbuzi Nchini na Teknolojia Walizonazo**

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK** aliuliza:-

Je, kuna Wavumbuzi wangapi na wa teknolojia gani kwani Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa una lengo la kuchochea uvumbuzi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Omar Kipanga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango wa uvumbuzi na ubunifu kama nyenzo muhimu katika kuchochea ushindani na uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya watu kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuibua, kutambua na kuendeleza uvumbuzi, ubunifu na maarifa asili ya Tanzania kupitia mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) na programu ya kutambua teknolojia zinazozalishwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imetambua wavumbuzi na wabunifu wapatao 2,735 katika sekta za Afya, Viwanda, Elimu, Kilimo, TEHAMA, Usafirishaji, Nishati, Madini, Mazingira, na Uvuvi. Aidha, Teknolojia 479 zimeweza kuibuliwa, kutambuliwa na kuhakikiwa. Wabunifu 376 wanaendelezwa na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* na Kati ya bunifu zilizoendelezwa, 35 zimefikia hatua za ubiasharishaji. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amour Hamis Mbarouk.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali ya nyongeza, lakini kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana mimi namuombea dua Mwenyezi Mungu amuongezee katika elimu yake hii. Ninayo maswali mawili.

Swali la Kwanza; Serikali inatumia sheria gani kuweka vigezo vya kuwatambua hawa wavumbuzi?

Swali la Pili; amesema kwamba kati ya wavumbuzi waliotambuliwa ni 2,735. Je, katika hawa Zanzibar wapo wangapi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amour, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Serikali imekuwa ikifanya mchakato wa kuibua hawa wabunifu, wabunifu hawa wanaibuliwa kwa mujibu wa Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 ambayo ilianzishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili kati ya wabunifu hawa 2,735 tumesema wabunifu 376 wanaendelezwa na Serikali, kati ya wabunifu hawa ni wabunifu 11 wanatoka upande wa Zanzibar. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki Mbunge wa Tarime Mjini.

Na. 75

**Darasa la Saba Kufanya Mtihani Mwezi wa Tisa**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, kwa nini darasa la saba wanafanya mtihani wa Taifa mwezi Septemba, wakati mtaala unaelekeza masomo yakamilike mwisho wa mwaka?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala wa elimu unaelekeza mwanafunzi kutumia siku 194 za mwaka kwa masomo. Aidha, mtaala wa elimu pamoja na

masuala mengine umezingatia muda wa kufanyika kwa mitihani ya ndani na ile ya Kitaifa. Hivyo, kukamilika kwa ufundishaji na ujifunzaji wa maudhui ya muhtasari kwa darasa la saba hutegemea zaidi mpango kazi wa Mwalimu. Kwa msingi huo, hadi kufika mwezi wa Septemba walimu wa darasa la saba hupaswa kuwa wamekamilisha kufundisha mada zilizobainishwa katika muhtasari ili kutoa nafasi ya ufanyikaji wa mitihani ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanyikaji wa mitihani ya kitaifa ya darasa la saba mwezi Septemba unasaidia kutoa nafasi kwa zoezi la usahihishaji na utoaji wa matokeo kwa wakati ili kutoa nafasi kwa wazazi na walezi kufanya maandalizi ya kuwawezesha watoto wao kujiunga na masomo ya ngazi nyingine za elimu ambapo masomo yanaanza Januari mwaka unaofuata. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Wizara imekuwa ikitoa tamko la kuzuia masomo ya ziada katika Shule za Msingi na ilhali wakijua kwamba muda wa ukamilishaji wa mtaala unakuwa hautoshi. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inatenga muda ambao watoto hao watasoma wakamilishe mtaala wao kwa wakati?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Walimu wanapaswa kutafuta muda wa kukamilisha mtaala huu kwa mpango kazi ambao wanao. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa motisha Walimu hawa ambao wanafanyakazi hii ngumu ya kuhakikisha kwamba elimu inatolewa kwa wakati? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kembaki Mbunge wa Tarime Mjini kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishajibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba katika mwaka tunazo siku 365, kati ya siku hizo 365 tunatumia siku 194 kwa ajili ya kukamilisha mitaala katika mwaka husika wa masomo. Najua maono ya Mheshimiwa Mbunge kwenye eneo hili, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa vile hivi sasa tunapitia Sheria yetu ya Elimu

tunapitia mitaala pia tunapitia sera ya elimu, bado hatujaona changamoto kwa hizi siku 194 kwenye utekelezaji wa mitaala hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa vile bado tunaendelea kubeba au kuchukua maoni tunaomba tubebe vilevile maelezo yake haya tuweze kuyaingiza kwenye rasimu yetu ya mitaala inayokuja ili tuweze kuangalia kama hizi siku 194 zitatosheleza au hazitatosheleza au kama kutakuwa na changamoto yoyote tuweze kufanya marekebisho. Hilo eneo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili la motisha, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekuwa ikitoa motisha au kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria. Kama tunavyofahamu katika kipindi kilichopita Mheshimiwa Rais aliongeza mshahara siyo tu kwa watumishi kama walimu, lakini kwa watumishi wote. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kufanya hivyo kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu ili watumishi wote waweze kupata stahiki zao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia kwa majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Juma Omar Kipanga tunashukuru sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili ya Utalii Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 76

**Wananchi Waliovamia Msitu wa Bondo – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaondoa wananchi waliovamia Msitu wa Bondo uliopo Kata ya Mswaki, Kijiji cha Mswaki?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu : -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti Hifadhi hii imekuwa ikivamiwa kwa ajili ya shughuli za kibinadamu zikiwemo kilimo, makazi na

kuchungia mifugo. Hadi sasa, Serikali imeweka matangazo ya kuwataka wavamizi wote kuondoka ndani ya Hifadhi hiyo ya Bondo kwa hiari yao ifikapo tarehe 30 Desemba, 2022.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri tu lakini nina maswali madogo mawili kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Bondo katika Kata ya Mswaki ni eneo muhimu sana kwa ajili ya mvua, halikadhalika kwa ajili ya mazingira. Lakini eneo hili ni la Serikali na lina GN 341 toka 1960. Swali langu je, nini mpango madhubuti na endelevu wa Serikali wa kulinda maeneo haya ili yasiweze kuvamiwa na wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; moja ya ahadi ya wenzetu wa *TFS* juu ya eneo hili walikuwa wajenge Kituo cha Afya lakini naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba tayari tumekuwa tukipata Milioni 500 Kituo cha Afya kwenye kijiji cha Mswaki kimejengwa. Je, nini kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wako tayari sasa kutujengea bwawa kwa ajili ya kitu kinaitwa *CSR*? Ahsante

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo ametoa ushirikiano kwetu kuhakikisha kwamba eneo hii tunalirudisha Serikalini, wananchi ni kweli walikuwa wamevamia eneo hili lakini kwa kutambua umuhimu wa hifadhi basi tumeanza kuwatoa hawa wavamizi na kuweka vigingi ili maeneo haya yaweze kutambulika rasmi kama ni eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango madhubuti wa Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo ni mazuri na ya muhimu katika kuhifadhiwa vizuri tumeendelea kutoa elimu kwa wananchi, na kwa kutambua kwamba wananchi pia ni sehemu ya uhifadhi, hivyo tumekuwa tukishirikiana na wananchi kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo tunayatambua na ni ya muhimu tunayahifadhi vizuri kwa maslahi ya Taifa. Kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wanatambua umuhimu wa uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala lingine ambalo amelisema la Kituo cha Afya, ni kweli Serikali iliwahi kuahidi kuwajengea Kituo cha Afya katika

Wilaya ya Kilindi katika Kijiji cha Mswaki na kwa bahati nzuri Serikali imetimiza ahadi hiyo. Kwa kuwa, tumekuwa tukitoa *CSR* katika maeneo mbalimbali ambayo yanazunguka maeneo yaliyohifadhiwa Mheshimiwa Mbunge nimuombe tulichukue ombi lake tuende tukachakate na hatimay tutampa majibu yaliyo sahihi lakini tuwahakikishie wananchi wa Kilindi na Mswaki kwamba tutahakikisha wanapata *CSR* kama moja ya wajibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Omari.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake.

Na. 77

**Umuhimu wa kujua bei ya kuuzia Tumbaku kabla ya kufunga mkataba wa uzalishaji Tumbaku**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini wakulima wasianze kujua bei ya kuuzia tumbaku na bei ya pembejeo kabla ya kufunga mkataba wa uzalishaji?

**MWENYEKITI:** Majibu wa swali hilo Naibu Waziri Mheshimiwa Antony Mavunde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Tumbaku Na. 24 ya mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2009 na kanuni za mwaka 2011, wakulima wa tumbaku wanapaswa kufunga mikataba ya uzalishaji wakiwa wanajua bei ya kuuzia tumbaku na bei ya pembejeo za kilimo. Huu ndio utaratibu uliopo unaoendelea kusimamiwa na Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania. Katika msimu wa mwaka 2022/2023, tayari wakulima wamepata bei ya tumbaku na pembejeo tangu tarehe 30 Agosti, 2022. Kutokana na masoko yaliyopatikana bei elekezi imepanda kutoka Dola za Marekani 1.65 mwaka 2021/2022 hadi Dola za Marekani mbili mwaka 2022/2023 kwa kilo ya tumbaku, sawa na ongezeko la asilimia 21.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nimuulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya kuuzia tumbaku ni muhimu sana kwa mkulima; je, wakulima wenyewe wanashirikishwaje katika kufikia uamuzi wa bei gani tumbaku yao iuzwe?

Swali la pili tunaishukuru Serikali kwa kutupa ruzuku, lakini naomba Serikali ituhakikishie sisi watu wa Urambo; je, mbolea ya tumbaku ni miongoni mwa mbolea zilizopata ruzuku? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu wa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushiriki wa wakulima, kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Tumbaku Namba 24 ya mwaka 2021 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2011 Kifungu cha 43 (1) kimeweka masharti ya ushiriki wa wakulima kupitia vyama vyao vikuu katika majadiliano ya bei na pembejeo. Hivyo, nidhahiri kwamba kupitia sheria hii wakulima wanashiriki kupitia vyama vyao vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu mbolea ya ruzuku; katika mwongozo ambao tumeutoa kwenye mbolea ya zuruku, mbolea ya ruzuku ni kwa mbolea zote ikiwemo mbolea ambazo zinahusiana na zao la tumbaku. Kule kwenye tumbaku wanatumia mbolea hasa za *NPK* na *CAN* ambapo hadi hivi sasa kwa mujibu wa maoteo ni jumla ya tani 37,000 zitahitajika na tayari zipo kwenye utaratibu huo kuingia kwenye suala hili la ruzuku.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Antony Mavunde Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 78

**Malengo ya Kuanzisha Chuo cha Diplomasia**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, ni yapi yalikuwa malengo ya Serikali kuanzisha Chuo cha Diplomasia?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Geophrey Pinda Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia hapo awali kilikuwa ni chuo cha kimkakati ambacho kilianzishwa kwa ushirikiano kati Tanzania na Msumbiji kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi mbalimbali katika nyanja za kidiplomasia na uongozi katika ngazi za kitaifa na kimataifa kutoka katika hizo nchi mbili. Kutokana na ubora cha chuo hiki Serikali ilifanya maboresho kwa kuongeza mitaala na kilianzisha kozi katika ngazi ya cheti, stashahada, shahada, stashahada ya uzamili na shahada ya uzamili ambazo zilianza kujumuisha wanafunzi kutoka nje ya mfumo wa watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa chuo kimezalisha wanadiplomasia wengi ambao wameweza kuajiliwa katika Serikali yetu, sekta binafsi pamoja na jumuiya za kikanda na kimataifa. Hivyo, chuo kimefikia lengo lake baada ya kufanyika kwa maboresho husika na kuweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya taifa letu na wananchi kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, wanafunzi wanaosoma Chuo cha Diplomasia wanafanya wapi mafunzo kwa vitendo ili sasa lengo la kuanzisha Chuo cha Diplomasia liwe limetimia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali imekubali kwamba yaliyokuwa malengo ya msingi kuanzia Chuo cha Diplomasia kwa sasa

yamebadilika kutokana na mahitaji ya nchi na pia kutokana na masuala mengine ambayo Serikali wanajua kwanini walipadilisha.

(b) Je, ni kwanini sasa Serikali isione haja ya kupitia upya mfumo wa utoaji elimu kwenye chuo hiki ambacho lengo lake lilikuwa ni kutoa viongozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu hata wanaotolewa katika chuo hiki wahitimu wengi hawatumiwi kama ambavyo lengo la kuanzisha chuo hicho lilivyokuwa. Sasa ni kwanini wasipitie upya ili wanaohitimu katika chuo hicho wawe na tija kwa taifa na Serikali ifikie malengo yake inayosema kwamba inazalisha viongozi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kuhusu mafunzo kwa vitendo. Chuo hiki kimsingi kinapowatoa wale wanafunzi wanakwenda kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya *field* zao, moja ya eneo ambalo wanapewa nafasi ni Wizara ya Mambo ya Nje yenyewe ambako wanafunzi wachache huwa wanapewa nafasi kutokana na ukweli wa uwezo wa Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maeneo mengine ni kwenye taasisi mbalimbali zenye sura ya Kimataifa, vile vile kule kwenye *NGO* na maeneo ambayo utendaji wake upo katika sura ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la tija, ni kwamba chuo hiki kina tija kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba kwa sasa kimezalisha wanadiplomasia wengi sana ambao wanatumika katika maeneo mbalimbali. Na ukizingatia kwamba tuna hiki chuo kiliboreshwa na kufanyiwa maboresho ya uhakika kimekuwa na sura ya chuo kikuu, na sasa hivi kinatoa hadi shahada ya juu, kama nilivyoieleza hapo, wanatoa hadi masters pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachoweza kusema ni kwamba mafunzo wka vitendo wanapatiwa lakini vile vile tija inaonekana kwenye Nyanja za kimataifa na wasomi wengi sana tumekuwa tukiwatumia katika maeneo mbalimbali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Geophrey Pinda kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tunaendelea na

Wizara ya Afya Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Hitaji la Madaktari Bingwa Hospitali ya Rufaa Rukwa**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa?

**MWENYEKITI:** Majibu wa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziriwa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa hadi sasa ina jumla ya Madaktari Bingwa watano wa fani za afya kama ifuatavyo; mama na uzazi wawili, magonjwa ya watoto wawili pamoja na madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani *(physician)* mmoja. Katika kuongeza idadi ya madaktari bingwa, Wizara imepeleka kusoma jumla ya madaktari watano kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa, ambao ni madaktari wawili wanasomea upasuaji, daktari mmoja anaesomea upasuaji wa mifupa, daktari mmoja anasomea magonjwa ya dharula na daktari mmoja anaesomea kinywa, sikio na koo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; wakati huwa tunasubiri madaktari waliokwenda kusoma lakini pia bado ile hospitali ni chakavu, na miundombinu yake imechoka; na wakati huo tuna eneo ambalo lilipimea na limefanyiwa usanifu.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili wakati huwa tuna changamoto za madaktari inalazimika wagonjwa kuwasafirisha kuwapeleka rufaa ya Mbeya.

Je, ni lini Serikali itaongeza magari kwenye hospitali ya Rufaa Mkoa wa Rukwa ikiwemo na *ambulance?* ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Bupe Mwakang'ata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza la kwamba wameshatenga eneo na kwamba ni lini Serikali itaanza ujenzi kwenye eneo jipya ambalo hospitali ya mkoa inataka kujengwa. Kwenye bajeti kwa mwaka huu imetengwa Bilioni tatu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali hiyo, pamoja na Shilingi milioni mia tisa kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye eneo lile ambalo sasa hivi bado majengo yake ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kwamba sasa hivi wagonjwa wanapekekwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, kwa maana ya rufaa wanapokuwa wanashida. Umeona idadi ya madaktari bingwa waliopo kwenye hospitali yako ya Mkoa. Maana yake ni nini, wanaopeleka rufaa Mbeya ni wale ambao wanahitaji kutibia kwenye hospitali ya *level* ya Kanda. Lakini tanategemea kwa idadi hii ya madaktari tulionao ambao sasa hivi katika hao watano waliopo shuleni watatu watamaliza mwezi ya kumi mwakani. Maana yake ni kwamba tutaongeza idadi ya madaktari bingwa na hata rufaa nayo itapungua, ili ifikie kwamba wale wanaohitajika kanda ndio waende lakini wa *level* ya mkoa ibadi pale pale mkoani. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Wizara ya Afya. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 80

**Kurekebisha Ramani ya Tanzania**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kurekebisha ramani ya nchi yetu baada ya baadhi ya maeneo kujazwa mchanga kuongeza ukubwa wa ardhi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Ridhiwani.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali namba 80 la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge, napenda kutoa maelezo mafupi kuwa, ukubwa wa eneo na mipaka ya nchi unajulikana na ipo bayana. Hivyo kujazwa mchanga kwenye baadhi ya maeneo hakuongezi wala kupunguza ukubwa wa eneo la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani ya nchi inaonesha sura ya nchi huandaliwa ili kuonyesha hali halisi iliyopo ardhini ikijumuisha taarifa za kijiografia za asili ambazo ni pamoja na mito, maziwa, milima na bahari; na zile zisizo za asili ambazo zinazojumuisha barabara, reli, mabwawa na miji. Moja ya sababu ya kuhuisha ramani ni kuonesha uhalisia wa sura ya nchi na kuhakikisha kuwa mabadiliko yanayotokea katika ardhi yanaoneshwa kwenye ramani mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango wa kuandaa ramani mpya nchi nzima zinazoonesha sura ya nchi Tanzania Bara. Ramani hizo zitaandaliwa kupita mipaka kupitia Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani *(Project for Improvement of National Land Data Infrastructure)* utakaotekelezwa kwa mkopo utakaotolewa na Serikali ya Korea kwa muda wa miaka minne (2022/23 -2025/2026).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rita Kabati swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kutokana na mabadiliko ya tabianchi mipaka mingi ya asili baina ya mikoa na mikoa, wilaya na wilaya, kata kwa kata, vijiji kwa vijiji, vitongoji kwa vitongoji imebadilika sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha sasa Mipaka hiyo ili iwe sawasawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali letu la pili. Je, ni nili huo mradi wa Korea utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo mafupi ya nyongeza ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Ritta Kabati kwa niaba ya Mheshimiwa Angelina Malembeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusiana na jambo la tabianchi, ni kweli ipo baadhi ya mito ya asili ambayo imekauka hivyo kusababisha migogoro katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na kulihakikishia Bunge lako kwamba Serikali imeshafanya zoezi la kutambua na kuchora ramani za mikoa hiyo, hivyo suala hilo litakapokuwa limetokea zipo hatua ambazo zimeshachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, juu ya ni lini mradi utaanza, nataka kulihakikishia Bunge lako kuwa, pale tutakapokuwa tumeshaandaa taratibu zote, ikiwemo kuweka ofisi na kupata wataalam wakaosimamia zoezi hilo, zoezi hilo litaanza.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete Naibu Waziri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Katiba Mheshimiwa, Kenneth Ernest Nollo Mbunge wa Bahi sasa aulize swali lake.

Na. 81

**Mikataba ya Madini na Nishati kujadiliwa Bungeni**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza kuleta mikataba ya madini na nishati ijadiliwe Bungeni kabla ya kuingia makubaliano na wawekezaji?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Geophrey Pinda Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi Sura ya 450 kifungu cha 5 inatoa wajibu wa Bunge kwa mujibu wa ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, katika utekelezaji wa jukumu lake la kuishauri Serikali linaweza kuitisha mikataba inayohusu masuala ya utajiri na rasilimali za nchi na kuweza kupitia kwa lengo la kuishauri Serikali na kutoa azimio la kuondoa masharti hasi katika mikataba. Takwa hili la sheria linazingatia misingi iliyowekwa na sheria, kwamba mikataba au makubaliano yaliyoingiwa kati ya Serikali na wawekezaji yanazingatia haki, usawa na nia njema kwa pande zote na kuzingatia maslahi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwasilisha mikataba kupitia kamati za kudumu za Bunge na Kamati kuzitolea maelekezo na ushauri kutoka kwa sekta husika. Pale Kamati husika inapoona umuhimu wa kufikisha mkataba mbele ya Bunge lako Tukufu maelekezo hutolewa na kwa kuzingatia Sheria husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo.

**MHE.KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo yanayolalamikiwa katika nchi zenye utajiri wa mafuta ya gesi ni kukosekana kwa utawala bora katika kuwa na uwazi kwa mikataba hii kwa umma; je, ipi mikakati ya Serikali katika kuenzi jitihada za kufikia lengo hili la kuwa na uwazi wa mikataba kwa ujumla katika umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili pamoja na kwamba mikataba imekuwa inakuja bungeni kupitia Kamati; je, Serikali haioni kama kuna umuhimu wa kubadilisha utaratibu huu ili kuwe na utaratibu ambao Bunge litaweza kuona kwa maana ya Bunge zima hata kuwe kwa kipindi cha mwisho wa mwaka ili waweze kuona ni maeneo gani ambayo Serikali imeingia mkataba na waweze kupata uelewa wa pamoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nollo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwazi katika mikataba upo na kimsingi kwa sababu muuliza swali ni sehemu ya Wabunge na Kamati za Bunge zimeundwa kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa Kibunge, zinapopata nafasi ya kupitia mikataba hii huwa ni kupunguza lile jambo katika mazingira ambayo yanaweza upotofu wa jumla katika suala la mikataba. Hivyo basi mikataba inapojadiliwa na Kamati za Bunge ni kisheria kabisa unakuwa tayari maelekezo yanayotolewa na Kamati zile yanakuwa ni halali na ni sawa kufikishwa mbele ya Bunge lako Tukufu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lile suala la kubadilisha mfumo, ni Bunge hili lililokaa na likaweka utaratibu huo, na ni Bunge hili hili linaweza likabadilisha mfumo. Hivyo basi ni jambo ambalo ningemshauri Mheshimiwa Mbunge kutoa hoja ili sasa vyombo vinavyohusika katika kubadilisha mifumo viweze kuchukua nafasi yake. Lakini kwa namna tunavyokwenda kwa sasa ni jambo ambalo linazingatia taratibu na sheria tulizojiwekea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Geofrey Pinda kwa majibu ya swali hilo.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na mipango Mheshimiwa Zahor Mohamed Haji, Mbunge wa Mwera, sasa aulize swali lake.

Na. 82

**Idadi na aina ya mikopo iliyokopwa na Zanzibar**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuza:-

Je, Serikali inaweza kutoa idadi na aina ya mikopo ya Zanzibar baada ya makubaliano na kuiwezesha Zanzibar kukopa yenyewe?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 15 cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepewa mamlaka ya kupokea misaada yenyewe kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mujibu wa kifungu cha 3 na 13, mamlaka ya kukopa na kutoa dhamana yamewekwa chini ya Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na anaweza kuyakasimu kwa Waziri wa Fedha wa SMZ baada ya kushauriwa na Kamati ya Kitaifa ya Madeni yenye Wajumbe toka pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, yaani 2019/2020 - 2021/2022, thamani ya mikataba ya mikopo kutoka vyanzo vya nje iliyosainiwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya SMZ ikiwemo barabara, afya, elimu na mapambano dhidi ya janga la UVIKO-19 ni takribani shilingi trilioni 1.1. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; je, Serikali sasa iko tayari kutoa taaluma hii baada ya mkanganyiko wa mambo haya kwa upande wa Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; je, lini hili linaweza kuanza kufanyika kwa ajili ya kuondoa huo mkanganyiko? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo mafupi ya nyongeza Mheshimiwa Naibu waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zahor kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada ya Serikali kutoa taaluma kwa wananchi wake na taasisi mbalimbali, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wote juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili anauliza, ni lini? Niseme, Serikali kutoa taaluma kwa wananchi wake ni suala endelevu. Kwa hiyo, tunaendelea kutoa taaluma kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Hamad Hassan Chande kwa majibu hayo. Tunaendelea na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 83

**_BoT_ Kutoa dhamana kwa waagizaji mbolea**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia mfuko uliopo *BoT* wa trilioni moja kutoa dhamana kwa waagizaji mbolea kwa njia ya *hedging/options?*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Agosti, 2021 *BoT* ilianzisha mkopo maalum wa shilingi trilioni 1.0 kwa benki na taasisi za kifedha ili kuziwezesha kutoa mikopo kwenye sekta ya kilimo ikiwemo mifugo, uvuvi na misitu. Kupitia mkopo huu, mkopaji anaruhusiwa kutumia kwa kununua au kuagiza mbolea na pembejeo za kilimo kwa utaratibu atakaoona unafaa ikiwemo *hedging or options*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza napenda nianze na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuanza utekelezaji wa kutoa ruzuku kwenye pembejeo za mbolea na zoezi hilo linaenda vizuri sana na wananchi wamepunguziwa mzigo mkubwa kwenye pembejeo za mbolea kupitia hiyo ruzuku pamoja na soko la dunia mbolea kupanda bei kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu; kwa sababu kimuundo Benki Kuu huwa inakopesha mabenki kwa muda mfupi na katika hali hiyo haiwezi kukidhi mahitaji ya mikopo ya kilimo ambayo ni ya muda mrefu. Sasa je, ni kwanini Serikali haioni kuhamisha huo mfuko kutoka Benki Kuu na kwenda Benki

ya Maendeleo ya Kilimo, hizo shilingi trilioni moja ziweze kusaidia wakulima? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Njeza kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalichukua na kulifanyia tathmini, tukiona kwamba upo ubora wa kufanya hivyo, Serikali itachukua hatua stahiki. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 84

**Matawi ya Benki ya Kilimo – Kagera**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA K.n.y. MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafungua Matawi ya Benki ya Kilimo katika Wilaya za Mkoa wa Kagera?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo *(TADB)* imefanikiwa kufungua matawi katika kanda tano ambazo ni Kanda ya Kati, Dodoma; Kanda ya Mashariki, Dar es Salaam; Kanda ya Magharibi, Tabora; Nyanda za Juu Kusini, Mbeya na Kanda ya Ziwa, Mwanza ambayo inahudumia Mkoa wa Kagera na wilaya zake. Aidha, Benki ipo katika hatua za mwisho za kufungua Ofisi ya Kanda ya Kusini, Mtwara na hatua za awali za kufungua Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha ufunguzi wa Ofisi za Kanda, *TADB* itaangalia uwezekano wa kufungua ofisi katika mikoa na ikiwezekana wilaya, lakini hili litazingatia uwezo wa benki wa kifedha ikiwa ni pamoja na faida na ukuaji wa mtaji. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa kwa niaba.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nikijaribu kupitia huku kwenye benki hii, ni takribani miaka 10 sasa tangu benki hii ianzishwe. Ilianzishwa mwezi Septemba, 2012, lakini tunaona ina matawi matano tu. Matawi haya matano yako katika majiji haya makubwa, lakini tunajua wakulima wako kwenye vijiji vyetu na kata zetu ambako tunatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, kwa sababu Serikali imesema itapanuka lakini *based on* kupata pesa ya mtaji mkubwa zaidi: Ni nini mpango wa Serikali kuiongezea pesa benki hii hata kupitia hazina ili wakulima wetu ambao wametutuma sisi hapa waweze kunufaika na benki hii ambayo ina miaka zaidi ya 10 lakini haijawafikia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: tarehe 9/6/2022 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa katika ziara ya Mkoa wa Kagera kwenye uwanja wa Kaitaba alitoa maelekezo maalum kwa Serikali ya Mkoa wa Kagera na akai-*cite* kwamba tumekuwa na shida ya mafuta ya kula katika nchi hii na mpango uliopo ni kuutumia Mkoa wa Kagera ambao una maeneo makubwa ambayo hayatumiki kwa ajili ya kufanya kilimo cha michikichi na kilimo cha alizeti; na ameelekeza tutenge hekta takribani 70,000 mpaka 100,000 kwa ajili ya kutatua tatizo hili:-

Sasa je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuielekeza benki hii pamoja na kwamba mtaji wao bado ni mdogo, ielekee Kagera ikaungane na Serikali ya Mkoa ili waone wanasaidiaje kutatua tatizo hili la mafuta ya kula? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eng. Ezra kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza tunalipokea kama ushauri na tunaenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili pia tunaenda kulifanyia tathmini tuone kama upo umuhimu wa kuelekea kwa wakati huu; na kwa kuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais kunyanyua uchumi katika Mkoa wa Kagera, basi nalo hili tumelipokea na tunalifanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza maswali yetu kwa siku ya leo na yafuatayo ni matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kuna wageni ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni wageni wa Bunge; kwanza ni Ndugu Haji Manara, Msemaji wa Mabingwa wa Tanzania *Young African Sports Club. (Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** *TFF* wamuachie.

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana, *order, order!*. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** *TFF* wamwachie.

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Karibu sana Ndugu Haji Manara ambaye ni Msemaji wa Mabingwa wa *Tanzania Young African. (Makofi)*

Pia tuna Ndugu Rushyna Athumani ambaye ni msaidizi wake, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Angola hiyo!

**MWENYEKITI:** Pia Waheshimiwa Wabunge kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wapo Bungeni leo hii, tunaomba wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana wageni wa Wabunge wetu. *(Makofi)*

Pia kuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanakwaya 28 kutoka Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dar es Salaam Mtaa wa Petro na Paul Mtume, Mwenge, Kijitonyama. Ndio hao hapo, karibuni sana katika Bunge letu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Pia tuna wanakwaya 44 wa KKKT Balali kutoka Kilolo Mkoani Iringa, karibuni sana wanakwaya wetu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Pia tuna tangazo la Wabunge wanawake *(TWPG)* kuwa kesho Jumanne tarehe 20 Septemba, 2022 kutakuwa na mahafali *(graduation)* ya kupokea vyeti kwa Wabunge Wanawake wote ambao walishiriki mafunzo yaliyotolewa na Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)* kuanzia tarehe 9 Mei hadi tarehe 3 Juni, 2022. Mahafali hayo yatafanyika mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Katibu tuendelee.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 *(The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie kwamba Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa mwaka 2022 *(The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill,2022)* uliosomwa kwa mara ya kwanza leo tarehe 19 Septemba, 2022 utapelekwa kwenye Kamati ya Bajeti ili ufanyiwe kazi. Aidha, Kamati ya Uongozi ilikaa na kuridhia Muswada huu ulioletwa kwa hati ya dharura uingie Bungeni siku ya Alhamisi tarehe 22 mwaka 2022 kwa ajili ya kusomwa kwa mara pili na hatua zake zote.

Waheshimiwa Wabunge, pia kulikuwa na tangazo ambalo lilikuwa nyuma ya huu Muswada ambapo Waheshimiwa Wabunge wanatangaziwa matokeo ya mechi zilizochezwa kwenye Bonanza la Michezo kati ya Bunge *Sports Club* na Benki ya *NMB* tarehe 17 Septemba, 2022 kama ifuatavyo:-

Mpira wa Kikapu, wanaume; *Bunge Sports Club* walishinda *set* 45 kwa 40. Mpira wa kikapu, wanawake; *Bunge Sports Club* walishinda. Mpira wa wavu, wanaume, *Bunge Sport Club* walishinda. Mpira wa wavu, wanawake *Bunge Sports Club* walishinda. Mpira wa pete, *Bunge Sports Club* walishinda magoli 29 kwa nne. *(Makofi)*

Mchezo wa kuvuta kamba, wanaume na wanawake; *Bunge Sports Club* walishinda pia; mchezo wa kukimbiza kuku, wanawake; *Bunge Sports Club* walishinda pia; mchezo wa kukimbiza kuku, wanaume; Benki ya *NMB* walishinda na mpira wa miguu; Benki ya *NMB* walishinda magoli mawili kwa sifuri.

Hivyo *Bunge Sports Club* walishinda makombe nane kati ya makombe kumi yaliyoshindaniwa. Hongereni sana *Bunge Sports Club*. *(Makofi)*

Katibu tuendelee.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004)***

**MWENYEKITI:** Sasa naomba nimwite Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili aweze kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 karibu sana Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Mataifa katika kutekeleza majukumu yake yanayohusu masuala ya Ulinzi na Usalama kwa kutumia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ulizitambua changamoto zinazosababisha uvunjifu wa amani na ukosefu wa usalama na kusababisha hofu kwa watu, vifo na majeruhi katika jamii duniani. Mojawapo ya sababu hizo ni vitendo vya kigaidi ambavyo hutekelezwa na watu au makundi ya watu wenye vurugu zinazotokana na misimamo mikali *(violent extremism)* ambao wanafadhili vitendo vya ugaidi kwa kutumia baadhi ya vijana ambao hubadilishwa kifikra na kuwa na msimamo mkali *(radicalization)* na kisha huwatumia katika kutenda matukio ya kigaidi ili kutimiza malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia changamoto hii ya ugaidi, Umoja wa Mataifa ulichukua hatua mbalimbali za kuzuia kuenea kwa vitendo vya kigaidi. Moja ya hatua hizo ni kutumia mikataba mbalimbali ambayo inatumika kuziunganisha nchi wanachama kuzuia uhalifu unaovuka mipaka kama njia za kutatua changamoto za Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ambalo limeendelea kutoa miongozo, taratibu, maazimio, mikataba, na matamko mbalimbali katika kushawishi nchi wanachama kuungana pamoja ili kuzuia na kupambana na ugaidi. Mfano ni Azimio Na. 1373 la mwaka 2001 na Mkakati wa

Dunia wa Kupambana na Ugaidi wa mwaka 2006 *(The United Nations Global Counter-Terrorism Strategy of 2006)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, nchi nyingi wanachama wa Umoja wa Mataifa, ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimesaini na kuridhia mikataba hii, Itifaki na maazimio na makubaliano mbalimbali ya kuzuia na kupambana na ugaidi. Baadhi ya mikataba, Itifaki na maazio hayo yametumika katika kutengeneza utaratibu wa namna ya kutekelezwa na kutungiwa sheria na kanuni kutegemea utaratibu wa nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zinasisitiza kushirikiana kupitia ushirikiano wa kikanda kuhakikisha kuwa migogoro na ugaidi inazuiwa na wahusika wake wanashughulikiwa kisheria kwa kutumia mbinu zote za kisheria na ushirikiano wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kupambana na changamoto ya ugaidi duniani, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa baada ya tukio la kushambuliwa kwa Balozi za Marekani zilizopo Afrika Mashariki katika nchi za Kenya na Tanzania tarehe 7 Agosti, 1998 na baada ya tukio la kushambuliwa kwa majengo pacha Jijini *New York* tarehe 11 Septemba, 2001 nchini Marekani kwa kutumia ndege za abiria, lilipitishwa Azimio Na. 1373 la Mwaka 2001 kupitia Ibara ya 7 ya Katiba ya Umoja wa Mataifa *(Action With Respect to Threats to The Peace, Breaches of The Peace, And Acts of Aggression)*. Ibara hii hutumiwa kupambana na matukio au changamoto zinazotishia uvunjifu wa amani na kuweza kusababisha vurugu za kivita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili lilitambuliwa na kupitishwa kwa maazimio mengine, ikiwemo Azimio namba 1269 la mwaka 1999, ambalo linaonesha kusikitishwa na ongezeko la vitendo vya ugaidi vinavyohatarisha maisha ya watu, amani na usalama wa nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa. Azimio hilo linalaani vitendo vya kigaidi bila kujali nia iliyochochea utekelezaji wa vitendo hivyo na mahali vilipofanyikia. Azimio hilo pia, linatoa maelekezo kwa Mashirika ya Kikanda ambapo katika Umoja wa Afrika ulipitisha Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa mwaka 1999 *(OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorisms)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia madhumuni ya mkataba huu ambao unahimiza ushirikiano kati ya Nchi Wanachama katika kuzuia na kupambana na ugaidi, Tanzania iliridhia mkataba huu tarehe 3 Septemba, 2003 na kuanza kutekeleza. Mwaka 2004, ilianzishwa Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention of Terrorism, 2004)* ikiwa ni katika kuzingatia ibara

ya 21(1) ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilisaini Itifaki hiyo tarehe 27 Januari, 2005. Aidha, kifungu cha 2 cha Itifaki hii kinarejea Ibara ya 3(d) ya Itifaki ya Kuanzisha Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika ya mwaka 2002 *(Protocol Relating to the Establishment of the Peace and Security Council of the African Union*, 9 July, 2002) kinazielekeza nchi kushirikiana katika kuzuia ugaidi. Aidha, Bunge la Tanzania lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002, Sura ya 19, ambayo ilifuatwa na kutungwa kwa Kanuni za Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2014. Sheria na kanuni hizi zimeandaliwa kwa misingi ya Mikataba na Itifaki iliyotajwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumeanza kuonekana dalili za baadhi ya wafuasi wa vikundi hivyo kuanza kuvuka mipaka na kuingia nchini kwa nia ya kuendeleza vitendo vyao vya kihalifu na kueneza itikadi za msimamo mkali za kuwashawishi watu kujiunga na makundi ya kigaidi. Hali hii inaifanya nchi yetu kuwa katika hatari ya kuathiriwa na harakati za vikundi vya kigaidi vinavyotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika tukio la kigaidi lililotokea nchini Uganda mwaka 2010, watuhumiwa wawili ambao ni raia wa Uganda walikamatwa nchini Tanzania na kurudishwa Uganda, kukabiliwa na mashtaka ya vitendo hivyo vya kigaidi. Kukamatwa na kusafirishwa kwa watuhumiwa hao kumefanyika kisheria na kwa kuzingatia mahusiano yanayotokana na mikataba ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sheria za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kumekuwa na matukio yenye viashiria vya ugaidi wa ndani ya nchi ambavyo vimejitokeza katika baadhi ya Mikoa ya Arusha, Geita, Mwanza, Pwani na Tanga. Hali hii inadhihirishwa na matukio ya kukamatwa kwa baadhi ya watuhumiwa waliokimbia baada ya kufanya vitendo vyenye viashiria vya ugaidi katika nchi jirani. Pia, kuna dalili za kuenea kwa itikadi ya misimamo mikali zinazopelekea watu kuhamasika na kujiunga na vikundi vya kigaidi na vikundi vyenye misimamo mikali nje ya nchi vinavyoweza kusababisha vitendo vya kigaidi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia mikataba na Itifaki za Kimataifa, Kikanda na Kitaifa, Tanzania inachukua hatua mbalimbali katika kupambana na ugaidi, kama vile kutungwa kwa Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002, kushirikiana na nchi jirani kulinda mipaka, kuanzisha Kituo cha Taifa cha Kuratibu Mapambano dhidi ya Ugaidi kinachoundwa na Maafisa kutoka vyombo vya ulinzi na usalama nchini na kuwa na mfumo mahsusi wa kutafuta, kuchakata na kubadilishana taarifa za kiintelijensia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia elimu imekuwa ikitolewa katika maeneo ya mikoa iliyotajwa kuwa na viashiria vya kigaidi ili wananchi wasishawishike kujiunga na vikundi au kufanya vitendo vya kigaidi. Hatua hii imesaidia kuwaelimisha wananchi kuelewa umuhimu wa kudumisha amani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii ina vipengele muhimu vifuatavyo ambavyo nchi yetu imevizingatia:-

(1) Ibara ya pili inayohusu malengo ya Itifaki. Lengo kuu la Itifaki ni utekelezaji wa ibara ya 21 ya Mkataba wa Umoja wa Nchi za Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ikiwa ni matakwa ya mkataba husika. Lengo lingine ni kuimarisha utekelezaji wa mkataba husika na kuwezesha utekelezaji wa Kifungu cha 3(d) cha Itifaki ya Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika *(Peace and Security Council)* katika kuratibu na kuoanisha jitihada za Umoja wa Afrika katika kuzuia na kupambana na ugaidi katika nyanja zote. Kwa kushirikiana na Nchi Wanachama, nchi yetu itaweza kulinda amani na usalama na kuhakikisha inaendelea kuimarisha ulinzi wa watu na mali zao.

(2) Ibara ya tatu ambayo inahusu majukumu ya Nchi Wanachama. Nchi Wanachama zinatakiwa kutekeleza vifungu vyote vya mkataba huu ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za lazima kulinda haki za msingi za binadamu dhidi ya vitendo vya kigaidi, kuzuia uingiaji na utoaji wa mafunzo kwa vikundi vya ugaidi katika nchi husika, kuainisha, kutambua na kuzuia au kukamata fedha na mali zilizotumika au zilizopangwa kutumika kwa ajili ya vitendo vya kigaidi na kuweka utaratibu wa kutumia fedha hizo kuwafidia waathirika wa vitendo vya kigaidi au familia zao; na kuanzisha vituo vya kitaifa kwa ajili ya kubadilishana na kupeana taarifa za makundi ya kigaidi kwa wakati na shughuli za kigaidi katika ngazi za kikanda, kibara na kimataifa.

Kupitia Itifaki hii Tanzania itaweza kupata taarifa na takwimu za wahusika wa vitendo vya kigaidi ndani na nje ya nchi kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Mapambano Dhidi ya Ugaidi. Pia, itawezesha kubadilishana wahalifu wa kigaidi kupitia makubaliano au mikataba maalum.

(3) Ibara ya nne, utaratibu wa utekelezaji wa Itifaki. Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika litakuwa na wajibu wa kuoanisha na kuratibu jitihada za Bara la Afrika katika kuzuia na kupambana

na ugaidi. Ibara hii inatoa fursa ya kuwa na utaratibu wa kubadilishana taarifa miongoni mwa Nchi Wanachama kuhusu makundi na mienendo ya vitendo vya kigaidi na kuimarisha mtandao wa kupashana habari katika ngazi ya Taifa, Kikanda na Kimataifa.

(4) Ibara ya tano ambayo ni wajibu wa Tume ya Umoja wa Afrika. Pamoja na mambo mengine, Tume itakuwa na wajibu wa kutoa msaada wa kitaalam kuhusu mambo ya kisheria na utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na masuala ya kupambana na ufadhili wa kifedha wa ugaidi, kuandaa miongozo itakayosaidia Nchi Wanachama kutunga sheria na mikakati ya kuzuia na kupambana na ugaidi katika nchi husika, kufuatilia Nchi Wanachama pamoja na utaratibu wa kikanda uliopitishwa na Baraza la Amani na Usalama na Taasisi nyingine za Umoja wa Afrika zinazohusiana na masuala ya ugaidi na kuendeleza na kudumisha kanzidata ya masuala yanayohusiana na ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii itawezesha nchi yetu kubadilishana utaalam na msaada wa kiufundi na kutumia kanzidata ya Kituo cha Afrika cha Masuala ya Ugaidi kilichopo Algiers nchini Algeria.

(5) Ibara ya sita ambayo inahusiana na wajibu wa jumuiya za kikanda katika utekelezaji wa Itifaki. Kuanzisha vituo vya mawasiliano juu ya masuala ya ugaidi katika ngazi ya kanda, kushirikiana na Tume ya Umoja wa Afrika katika kuanzisha na kuendeleza mikakati ya kuzuia na kupambana na ugaidi na kuhamasisha ushirikiano katika ngazi ya kanda juu ya utekelezaji wa Itifaki hii. Ibara hii itawezesha kuoanisha na kuratibu juhudi zetu za kitaifa katika kuzuia na kupambana na ugaidi kwa kushirikiana na Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* tayari tumeanzisha Kituo cha Kikanda cha Kupambana na Ugaidi *(SADC Regional Counter-terrorism Centre)*. Pia katika ukanda wa Afrika Mashariki, juhudi za kuanzisha Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Kupambana na Ugaidi *(EAC Counter-terrorism Centre)* kwa malengo ya kubadilishana taarifa za kiintelijensia na ujuzi katika kuzuia vitendo vya kigaidi.

(6) Ibara ya saba kuhusu utatuzi wa migogoro. Migogoro au tofauti yoyote itakayojitokeza baina ya Nchi Wanachama kuhusu tafsiri au

matumizi ya vifungu vya Itifaki hii utatatuliwa nje ya mahakama kupitia mashauriano ya Nchi Wanachama zinazohusika na mgogoro huo. Itifaki hii itatoa fursa kwa kutumia njia mbalimbali za usuluhushi endapo kutatokea migogoro kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Itifaki zikiwemo: Majadiliano baina ya nchi husika kwenye Mahakama ya Umoja wa Afrika ambayo itakuwa na mamlaka ya mwisho ya usuluhishi wa migogoro na Mahakama za Kimataifa kwa ajili ya usuluhishi kwa kuzingatia sheria za nchi.

(7) Ibara ya nane kuhusu kubadilishana wahalifu. Itifaki hii inaeleza kuwa Mikataba ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa mwaka 1999 utaweka utaratibu wa kisheria wa kubadilishana wahalifu kwa nchi ambazo hazina utaratibu huo. Endapo kutajitokeza migogoro kati ya Nchi mbili Wanachama zenye makubaliano au utaratibu wa kubadilishana wahalifu kati ya nchi hizo, vifungu vya mkataba huo vinavyohusu kubadilishana wahalifu vitatumika. Nchi yetu itaweza kutumia Itifaki hii kama msingi wa kisheria katika kuanzisha makubaliano na Nchi Wanachama kubadilishana wahalifu wa kigaidi.

(8) Ibara ya 10, kuanza kutumika kwa Itifaki. Kifungu hiki kinaeleza kuwa Itifaki hii itaanza kutumika siku 30 baada ya nchi ya 15 kuwasilisha hati ya kuridhia. Kimsingi Itifaki hiyo imeanza kutumika tarehe 27 Januari, 2014 kwa Nchi Wanachama wa *OAU* ambazo zimeshasaini na kuridhia.

(9) Ibara ya 11 ambayo inahusu utaratibu wa kufanya marekebisho ya kiitifaki. Nchi yeyote mwanachama inaweza kupendekeza marekebisho ya Itifaki hii kwa kuwasilisha mapendekezo yake kwa maandishi kwenye Tume ya Umoja wa Afrika ambapo itasambaza mapendekezo hayo kwa Nchi zote Wanachama. Marekebisho hayo yataidhinishwa kwa wingi wa kura za Nchi Mwanachama na yataanza kutumika kwa nchi husika zilizoridhia miezi mitatu baada ya Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika kupokea notisi ya kukubali. Endapo kutakuwa na mabadiliko ya sheria au masuala mengine yanayokinzana na maslahi ya Taifa, nchi yetu itaweza kuwasilisha mapendekezo ya kurekebisha Itifaki hii kwenye Tume ya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa ambayo nchi yetu itapata baada ya kuridhia Itifaki hii ni pamoja na yafuatayo:-

(1) Kuimarika kwa ulinzi na usalama wa raia na mali zao;

(2) Kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijinsia zinazohusu ugaidi kupitia ushirikiano na nchi wanachama;

(3) Kuongeza ujuzi kwa wataalam wetu kupitia ubadilishanaji wa uzoefu na mafunzo;

(4) Kuimarika kwa ushirikiano katika masuala ya urejeshwaji wa watuhumiwa wa ugaidi;

(5) Kuwezesha nchi yetu kushirikiana na nchi wanachama kulinda amani na usalama na kuhakikisha inalinda maisha ya watu na mali;

(6) Kuwezesha kubadilishana wahalifu wa kigaidi kupitia makubaliano au mikataba maalum;

(7) Kuwa na utaratibu wa kubadilishana taarifa miongoni mwa Nchi Wanachama kuhusu makundi na mienendo ya vitendo vya kigaidi na kuimarisha mtandao wa kupashana habari katika ngazi ya Taifa, kikanda na kimataifa;

(8) Kubadilishana utaalam na misaada ya kiufundi;

(9) Kuweza kutumia kanzidata ya Kituo cha Afrika cha masuala ya ugaidi kilichopo Algiers, Algeria;

(10) Kutumia njia mbalimbali za usuluhushi endapo kutatokea mgogoro kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Itifaki;

(11) Kutumia Itifaki hii kama mwongozo wa kisheria katika kuanzisha makubaliano na nchi wanachama ambazo hazina utaratibu wa kubadilishana wahalifu wa kigaidi; na

(12) Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kutokana na kuwepo kwa amani na usalama nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Itifaki husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe Itifaki kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ambao ulianzishwa tarehe 25 Mei, 1963 *(The Charter for Establishment Organization of African Unit, signed on 25th May, 1963)* kwa lengo kuu la kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika;

Na kwa kuwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zilipitisha mikataba na Itifaki mbalimbali zinazohusu amani na usalama ili kuendeleza utangamano na ushirikiano katika kuzuia na kupambana na ugaidi unaohatarisha hali ya usalama katika baadhi ya Nchi Mwanachama;

Na kwa kuwa moja ya mikataba iliyopitishwa ni Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 1999 na Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 2004 *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention of Terrorism of 2004);*

Na kwa kuwa madhumuni ya Mkataba huu ambao unahimiza ushirikiano kati ya Nchi Wanachama katika kuzuia na kupambana na ugaidi, Tanzania iliridhia mnamo tarehe 3 Septemba, 2003 na kuanza kuutekeleza;

Na kwa kuwa mwaka 2004 kama ilivyoelezwa katika ibara ya 21(1) ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa mwaka 1999, ulioanzisha Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa mwaka 2004 na kusainiwa na nchi yetu tarehe 27 Januari, 2005;

Na kwa kuwa ibara ya pili ya Itifaki hii inarejea ibara ya 3(d) ya Itifaki ya Kuanzisha Baraza la Amani la Usalama la Umoja wa Afrika ya mwaka 2002 *(Protocol Relating to the Establishment of Peace and Security Council of the African Union, July 9, 2002)* inazielekeza nchi kushirikiana katika kuzuia ugaidi.

Na kwa kuwa Bunge la Tanzania mwaka 2002 lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19 ambayo ilifuatiwa na kutungwa kwa Kanuni za Kuzuia Ugaidi za Mwaka 2014 na sheria ya kanuni hizi kutungwa na kuzingatia misingi iliyomo katika Mkataba na Itifaki mbalimbali za Umoja wa Kimataifa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika.

Hivyo basi kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Nchi Wanachama, Bunge hili katika Mkutano wa Nane na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya Pili, linaazimia kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika *(OAU)* wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa mwaka 2004 *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating Terrorism of 2004)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Injinia Hamad Yussuf Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa wasilisho hilo la kutaka Bunge kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004.

Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili aje atoe maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi mwaka 2004.

Karibu sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Vita Kawawa. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004 *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism of year 2004)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Juni, 2020, kimeielekeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kusimamia Wizara tatu

ambazo ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge za Kudumu, Toleo la Juni, 2020, kinazipa Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii jukumu la kushughulikia Miswada ya Kisheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na majukumu ya Kikanuni la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu, tarehe 16 Septemba, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Itifaki ya Umoja wa Nchi huru za Afrika *(OAU)* ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati ilipewa maelezo kuhusu vipengele vyote muhimu na faida za kuridhia Mkataba huo. Baada ya maelezo hayo, Kamati ilipata fursa ya kutafakari na kujadili kwa kina hoja hiyo ya Serikali na kuifanyia maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za Kimataifa, Kikanda na Kitaifa za kuzuia na kupambana na ugaidi kwa kuzingatia wajibu wa Kamati katika kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, Kamati ilipitia Machapisho mbalimbali kuhusu jitihada zilizofanyika Kimataifa, Kikanda na Kitaifa katika kuzuia na kupambana na ugaidi. Mapitio hayo yaliwawezesha Wajumbe kupata uelewa mpana kuhusu juhudi zilizokwisha fanyika na kuoanisha na Itifaki iliyowasilishwa mbele yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa Ugaidi umeendelea kuwa tishio la amani na usalama na kuathiri shughuli za kiuchumi na maendeleo za Mataifa mengi. Matukio hayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kuanzia Miaka ya 1990, ambapo matukio makubwa yaliyotingisha Jumuiya ya Kimataifa yalibadilisha mwelekeo wa kukabiliana na matukio ya kigaidi. Matukio hayo ni pamoja na kushambuliwa kwa Balozi za Marekani zilizopo Afrika Mashariki katika nchi za Tanzania na Kenya Mwaka 1998 na kushambuliwa kwa Majengo Pacha ya Kibiashara - *World Trade Centre* Jijini *New York* Marekani Septemba 11, 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya matukio hayo juhudi mbalimbali za Kimataifa, Kikanda na Kitaifa zimefanyika katika eneo la Amani na Usalama *(Peace and Security)* ili kuendeleza utangamano na ushirikiano katika kuzuia na kupambana na Ugaidi unaohatarisha hali ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya Kimataifa, Umoja wa Mataifa ulipitisha Miongozo mbalimbali ikiwemo Mikataba, Maazimio ya Baraza la Usalama *(United Security Council)* pamoja na Mpango Mkakati wa Dunia wa Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 2006 *(The United Nations Global Counter - Terrorism Strategy of 2006)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba ambayo ilipitishwa na Umoja wa Mataifa ni kama na ifuatayo: -

*(i)* *Convention on the Prevention and Punishment of Crimes against Internationally Protected Persons, Including Diplomatic Agents of the 1973;*

*(ii)* *International Convention against the taking of Hostages of 1979;*

*(iii)* *International Convention for the Suppression of Terrorist Bombings of 1997;*

*(iv)* *International Convention for the Financing of Terrorism 1999; na*

*(v)* *International Convention for the suppression of Acts of Nuclear Terrorism of year 2005.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa *(United Security Council)* lilipitisha Azimio 1373 *(United National Security Council Resolution 1373) Threat to International Peace and Security caused by Terrorist Act,* 2001. Ikiwemo Azimio la kihistoria ambalo lilifafanua kwa mapana wajibu wa Umoja wa Kimataifa katika kupambana na Ugaidi. Azimio hili lilipitishwa baada ya tukio la ugaidi la Septemba 11, 2001. Baada ya hapo Baraza lilipitisha Azimio 1624 - *Threats to International Peace and Security* 2005) na Azimio 2178 - *Threats to International Peace and Security caused by Terrorist Acts* 2014 yote yakiwa yanalenga kuzuia na kupambana na Ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maazimio, Mikataba na Itifaki hizo za Kimataifa, kiujumla zinasisitiza nchi wanachama kushirikiana kupitia Kanda zao kuhakikisha kuwa migogoro na ugaidi inazuiwa na wahusika wake wanashughulikiwa kisheria kwa kutumia mbinu zote za kisheria na ushirikiano wa nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kikanda, Kanda ya Afrika kupitia Umoja wa Afrika *(AU)* imekuwa ikifanya harakati mbalimbali za kuzuia na kupambana na ugaidi tangu umoja huu ulipokuwa ukijulikana kama Umoja wa Nchi huru za Afrika *(OAU)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miongo Minne, Kanda ya Afrika imekuwa ikipambana katika kuzuia vitendo vya ugaidi vinavyofanywa na makundi mbalimbali yakiwemo Alqaida, Al-Shabaab, Boko Haram na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa, katika kuzuia na kupambana na Ugaidi, Kanda ya Afrika imekuwa na miongozo mbalimbali ikiwemo ifuatayo:-

(i) *OAU Convention for the Elimination of Mercenarism*,1977 iliyoanza kutumika Mwaka 1985;

(ii) *OAU Resolution on the Strengthening of Cooperation and Coordination among African States* of the year 1992 ambapo nchi wanachama zilikubaliana kupambana dhidi ya msimamo mkali *(Extremism)* na Ugaidi *(Terrorism);*

(iii) *The OAU Assembly's Declaration on the Code of Conduct for Inter-African Relations* of the year 1994 ambapo Umoja wa Nchi Huru za Afrika ulipinga aina zote za msimamo mkali na ugaidi vinavyochangiwa na udini, udhehebu au ukabila;

(iv) *OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism* 1999 na kuanza kutumika mwaka 2002. Huu ndio Mwongozo Mkuu wa Nchi Huru za Afrika uliopitishwa kwa ajili ya kuzuia na kupambana na ugaidi ambao ndio ulipelekewa kuandaliwa kwa Itifaki ya Kuzuia na kupambana na ugaidi, ya Mwaka 2004;

(v) *Africa Union Plan of Action on the Prevention and Combating of Terrorism of year 2002* ambayo inaongeza nguvu ya kutekeleza Mkataba wa Mwaka 1999;

(vi) *PAP decision on the Prevention and Combating of Terrorism* of year 2010;

(vii) *African Centre for the Study and Research on Terrorism* kilichoanzishwa mwaka 2002 Nchini Algeria kwa ajili ya kuendeleza utafiti na kukuza uelewa kuhusu masuala ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kitaifa, Bunge la Tanzania lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002 Sura ya 19 na kutungiwa Kanuni zake mwaka 2014. Kamati ilijiridhisha kuwa Sheria hii na Kanuni hizi ziliandaliwa kwa misingi ya Mikataba na Itifaki za Kimataifa na Kikanda zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004, ilianzishwa kupitia Ibara ya 21(1) ya Mkataba wa Umoja wa Nchi huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa mwaka 1999, ambapo Tanzania iliridhia mwaka 2003. Aidha, Tanzania ilisaini Itifaki hii tarehe 27 Januari, 2005 ikiwa ni moja kati ya nchi 45 zilizotia saini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilibaini kuwa Ibara ya 2 ya Itifaki hii inarejea Ibara ya 3(d) ya Itifaki ya Kuanzisha Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika ya Mwaka 2002 *(Protocol Relating to the Establishment of the Peace and security Council of the African Union, of the year 2002)* ambayo inazielekeza nchi kushirikiana katika kuendeleza mapambano dhidi ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii, katika kuendeleza vita dhidi ya ugaidi kwa mujibu wa Itifaki na Mikataba ambayo Tanzania imekwisha saini na kuridhia, Bunge letu lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya Mwaka 2002 na kutungiwa Kanuni zake kuzuia Ugaidi za Mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia kwa kina vipengele vya Itifaki hiyo ili kubaini maudhui mahsusi ya Itifaki hiyo. Lengo ilikuwa ni kuelewa maudhui hayo na kuoanisha na mazingira ya Tanzania na hivyo kuweza kulishauri Bunge lako ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya ujumla ya Itifaki hiyo ni kuendeleza utangamano na ushirikiano wa nchi wanachama katika kuzuia matukio na vitendo vya ugaidi na hivyo kuendelea kudumisha amani na usalama katika nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Aidha, kupitia Itifaki hii nchi wanachama ikiwemo Tanzania zitawajibika:-

(i) Kuchukua hatua za lazima kulinda haki za msingi za binadamu dhidi ya vitendo vya kigaidi;

(ii) Kuzuia uingiaji na utoaji wa mafunzo kwa vikundi vya ugaidi katika nchi husika;

(iii) Kuainisha, kutambua na kuzuia au kukamata fedha na mali zilizotumika au zilizopangwa kutumika kwa ajili ya vitendo vya

kigaidi na kuweka utaratibu wa kutumia fedha hizo kuwafidia waathirika wa vitendo vya kigaidi au familia zao; na

(iv) Kuanzisha vituo vya Kitaifa kwa ajili ya kubadilishana na kupeana taarifa za makundi ya kigaidi kwa wakati na shughuli za kigaidi katika ngazi za Kikanda, Kibara na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilibaini kuwa kupitia Itifaki hii nchi wanachama ikiwemo Tanzania, zitaweza kupata taarifa na takwimu sahihi za wahusika wa vitendo vya kigaidi ndani na nje ya nchi. Pia, itawezesha nchi kubadilishana wahalifu wa kigaidi kupitia makubaliano au mikataba maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maudhui ya Itifaki hiyo, Kamati ilijiridhisha kuwa Itifaki hii ina tija kwa nchi yetu ambayo si kisiwa, kwa kuwa tumekuwa na matishio ya viashiria vya vitendo vya ugaidi ndani ya nchi. Mathalan, matishio ya viashiria vya ugaidi vimetokea katika Mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Arusha, Tanga, Mwanza, Geita na Pwani. Vitendo hivi vinachangiwa na baadhi ya wafuasi wa vikundi vya Kigaidi nje ya nchi kuvuka mipaka na kuingia nchini kwa lengo la kuendeleza vitendo hivyo vya kihalifu ikiwa ni pamoja na kueneza itikadi za msimamo mkali zinazopelekea watu kujiunga na makundi ya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilijiridhisha kuhusu nchi ambazo zimekwisharidhia Itifaki hii ambapo nchi 21 zimefanya hivyo. Kwa Afrika Mashariki nchi za Burundi na Rwanda pekee ndiyo zimekwisharidhia kati ya nchi Saba zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuridhia itifaki hii. Baada ya uchambuzi wa kina wa vifungu vya Itifaki hii kwa kuoanisha na matakwa ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 1999, Kamati imebaini kuwa zipo faida ambazo Tanzania itazipata kwa kuridhia Itifaki hii. Faida hizo ni pamoja na: -

(i) Kuimarika kwa Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao;

(ii) Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kutokana na kuwepo kwa amani na usalama nchini;

(iii) Kuwezesha nchi yetu kushirikiana na nchi wanachama kulinda amani na usalama na kuhakikisha inalinda maisha na mali za watu wake;

(iv) Kuwezesha kubadilishana wahalifu wa kigaidi kupitia makubaliano au mikataba maalum;

(v) Kuwa na utaratibu wa kubadilishana taarifa miongoni mwa nchi wanachama kuhusu makundi na mienendo ya vitendo vya kigaidi na kuimarisha mtandao wa kupashana habari katika ngazi ya Taifa, Kikanda na Kimataifa;

(vi) Kuweza kutumia kanzidata ya Kituo cha Afrika cha masuala ya ugaidi kilichopo Algiers - Algeria;

(vii) Kutumia njia mbalimbali za usuluhushi endapo kutatokea mgogoro kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Itifaki;

(viii) Ktumia Itifaki hii kama mwongozo wa kisheria katika kuanzisha makubaliano na nchi wanachama ambazo hazina utaratibu wa kubadilishana wahalifu wa kigaidi;

(ix) Kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijinsia zinazohusu ugaidi kupitia ushirikiano na nchi wanachama;

(x) Kuongeza ujuzi kwa wataalam wetu kupitia ubadilishanaji wa uzoefu na mafunzo na misaada kiufundi;

(xi) Kuimarika kwa ushirikiano katika masuala ya urejeshwaji wa watuhumiwa wa ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kujadili kwa kina hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004, Kamati inatoa maoni na Ushauri ufuatao:-

Moja; Bunge liridhie Itifaki hii kwa kuzingatia faida zitakazopatikana kutokana na uridhiwaji wa Itifaki hii;

Mbili; kwa kuwa Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002 ni ya siku nyingi ikilinganishwa na matukio ya ugaidi ambayo yanaongezeka kila siku, Sheria hii ifanyiwe marekebisho ili iendane na hali ya sasa. Aidha, Sheria hii iwe ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi na sio tu sheria ya kuzuia ugaidi, Sheria iendane kama ambavyo Mikataba na Itifaki nyingi zinavyotaja yaani *Prevention and Combating of Terrorism;*

Tatu; udhibiti wa uhalifu katika jamii ni vema ukaanzia katika ngazi ya familia, kaya, kitongoji na mtaa, kwa kujengewa uelewa na umuhimu wa kutoa taarifa za uhalifu. Hivyo, Serikali iimarishe mifumo ya utaoaji wa taarifa za kiharifu kuanzia ngazi ya familia;

Nne; kupitia Bunge lako Tukufu, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao hawajaridhia Itifaki hiyo washauriwe kufanya hivyo ili kuimarisha usalama wa Jumuiya hii;

Tano; kwa kuwa ukuaji wa uchumi unategemea usalama katika nchi, Serikali iandae Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ambao utaainisha hatua ambazo Taifa litachukua katika kuzuia na kupambana na Ugaidi, ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu elimu kwa umma na umuhimu wa kutoa taarifa kuhusu mienendo yenye mashaka ya watu, mitaala kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari ihusuyo mapambano dhidi ya ugaidi, uzingatiaji wa mgawanyo sawa wa rasilimali katika jamii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kuleta hoja hii kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili iweze kulifanyia kazi, jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Hamad Masauni, Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini Mbunge, Katibu Mkuu Ndugu Christopher Kadio, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano katika kipindi ambacho Kamati ilikuwa ikishughulikia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa weledi, uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wanafanya kazi ya Itifaki hii. Naomba Majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu rasmi za Bunge *(Hansard)* pamoja na taarifa yote hii niliyowasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi – *ndc,* kwa uongozi thabiti uliofanikisha uchambuzi wa

Itifaki huu na uratibu wa shughuli za Kamati. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein - *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria Ndugu Pius Mboya. Kipekee kabisa nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Ndugu Victoria Mizengo wakisaidiwa na Ndugu Rehema Kimbe waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hili na naomba Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki hii kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.*(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA MKATABA WA UMOJA WA NCHI HURU ZA AFRIKA (OAU) YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA UGAIDI YA MWAKA 2004 *(PROTOCOL TO THE OAU CONVENTION ON THE PREVENTION AND COMBATING OF TERRORISM OF 2004)* -**
**KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 60 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU) ya kuzuia na kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism of 2004)*.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, kimeelekeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kusimamia Wizara tatu (3) ambazo ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, kinazipa Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na jukumu la Kikanuni la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya

Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huu, tarehe 16 Septemba, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Mhe. Hamad Yussuf Masauni, (MB), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Itifaki ya Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU) ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004.

Vilevile, Kamati ilipewa maelezo kuhusu vipengele vyote Muhimu na faida za kuridhia Mkataba huo. Baada ya maelezo hayo, Kamati ilipata fursa ya kutafakari na kujadili kwa kina Hoja hiyo ya Serikali na kuifanyia maamuzi.

## 2.0 JITIHADA ZA KIMATAIFA, KIKANDA NA KITAIFA ZA KUZUIA NA KUPAMBANA NA UGAIDI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia wajibu wa Kamati katika kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, Kamati ilipitia Machapisho mbalimbali kuhusu jitihada zilizofanyika Kimataifa, Kikanda na Kitaifa katika kuzuia na kupambana na ugaidi. Mapitio hayo yaliwawezesha Wajumbe kupata uelewa mpana kuhusu juhudi zilizokwisha fanyika na kuoanisha na Itifaki iliyowasilishwa mbele yake.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa Ugaidi umeendelea kuwa tishio la amani na usalama na kuathiri shughuli za kiuchumi na maendeleo za Mataifa mengi. Matukio hayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kuanzia Miaka ya 1990, ambapo matukio makubwa yaliyotingisha Jumuiya ya Kimataifa yalibadilisha mwelekeo wa kukabiliana na Matukio ya Ugaidi. Matukio hayo ni pamoja na kushambuliwa kwa Balozi za Marekani zilizopo Afrika Mashariki katika nchi za Tanzania na Kenya Mwaka 1998 na kushambuliwa kwa Majengo Pacha ya Kibiashara *(World Trade Centre)* jijini New York Marekani tarehe 11 Septemba, 2001.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya matukio hayo juhudi mbalimbali za Kimataifa, Kikanda na Kitaifa zimefanyika katika eneo la Amani na Usalama *(Peace and Security)* ili kuendeleza utangamano na ushirikiano katika kuzuia na kupambana na Ugaidi unaohatarisha hali ya usalama.

**Mheshimiwa Spika,** katika ngazi ya Kimataifa, Umoja wa Mataifa (UN) ulipitisha Miongozo mbalimbali ikiwemo Mikataba, Maazimio ya Baraza la Usalama *(UN Security Council)* pamoja na Mpango Mkakati wa Dunia wa Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 2006 *(The United Nations Global Counter - Terrorism Strategy of 2006)*.

**Mheshimiwa Spika,** Mikataba ambayo ilipitishwa na UN ni pamoja na ifuatayo:-

i) *Convention on the Prevention and Punishment of Crimes against Internationally Protected Persons, Including Diplomatic Agents (1973)*

ii) *International Convention against the taking of Hostages (1979)*

iii) *International Convention for the Suppression of Terrorist Bombings (1997)*

iv) *International Convention for the Financing of Terrorism (1999)*

v) *International convention for the suppression of Acts of Nuclear Terrorism (2005)*.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN Security Council) lilipitisha Azimio 1373 (*UNSCR 1373 threats to international peace and security caused by terrorist acts)* Mwaka 2001, ikiwa ni Azimio la kihistoria ambalo lilifafanua kwa mapana wajibu wa Umoja wa Kimataifa katika kupambana na Ugaidi. Azimio hili lilipitishwa baada ya tukio la ugaidi la Septemba 11, 2001.Baada ya hapo Baraza lilipitisha Azimio 1624 *(Threats to International Peace and Security)* Mwaka 2005 na Azimio 2178 *(Threats to International Peace and Security caused by Terrorist Acts)* mwaka 2014 yote yakiwa yanalenga kuzuia na kupambana na Ugaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Maazimio, Mikataba na Itifaki hizo za Kimataifa, kiujumla zinasisitiza nchi wanachama kushirikiana kupitia Kanda zao kuhakikisha kuwa migogoro na ugaidi inazuiwa na wahusika wake wanashughulikiwa kisheria kwa kutumia mbinu zote za kisheria na ushirikiano wa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Kikanda, Kanda ya Afrika kupitia Umoja wa Afrika (AU) imekuwa ikifanya harakati mbalimbali za kuzuia na kupambana na Ugaidi tangu umoja huu ulipokuwa ukijulikana kama Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU).

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda wa miongo minne, Kanda ya Afrika imekuwa ikipambana katika kuzuia vitendo vya ugaidi vinavyofanywa na Makundi mbalimbali yakiwemo Alqaida, Al Shabaab, Boko Haram na mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, katika kuzuia na kupambana na Ugaidi, Kanda ya Afrika imekuwa na miongozo mbalimbali ikiwemo ifuatayo:-

i) *OAU Convention for the Elimination of Mercenarism* (1977) iliyoanza kutumika Mwaka 1985;

ii) *OAU Resolution on the Strenghtening of Cooperation and Coordination Among African States* (1992) ambapo Nchi wanachama zilikubaliana kupambana dhidi ya msimamo mkali *(Extremism)* na Ugaidi *(Terrorism);*

iii) *The OAU Assembly's Declaration on the Code of Conduct for Inter- African Relations* (1994) ambapo Umoja wa Nchi huru za Afrika ulipinga aina zote za msimamo mkali na ugaidi vinavyochangiwa na Udini, udhehebu au ukabila;

iv) *OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism* (1999) na kuanza kutumika 2002. Huu ndio Muongozo Mkuu wa Nchi Huru za Afrika uliopitishwa kwa ajili ya kuzuia na kupambana na Ugaidi ambao ndio ulipelekewa kuandaliwa kwa Itifaki ya Kuzuia na kupambana na Ugaidi, ya Mwaka 2004;

v) *Africa Union Plan of Action on the Prevention and Combating of Terrorism (2002)* ambayo inaongeza nguvu ya kutekeleza Mkataba wa Mwaka 1999;

vi) *PAP Decision on the Prevention and Combating of Terrosism* (2010);

vii) *African Centre for the Study and Research on Terrorism* kilichoanzishwa Mwaka 2002 Nchini Algeria kwa ajili ya kuendeleza utafiti na kukuza uelewa kuhusu masuala ya Ugaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Kitaifa, Bunge la Tanzania lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya Mwaka 2002 Sura ya 19, na kutungiwa Kanuni zake Mwaka 2014. Kamati ilijiridhisha kuwa Sheria hii na Kanuni hizi ziliandaliwa kwa misingi ya Mikataba na Itifaki za Kimataifa na Kikanda zilizotajwa hapo juu.

## 3.0 ITIFAKI YA MKATABA WA UMOJA WA NCHI HURU ZA AFRIKA (OAU) YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA UGAIDI YA MWAKA 2004 *(PROTOCOL TO THE OAU CONVENTION ON THE PREVENTION AND COMBATING OF TERRORISM OF 2004)*

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004, ilianzishwa kupitia Ibara ya 21 Ibara Ndogo ya 1 ya Mkataba wa Umoja wa Nchi huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 1999, ambapo Tanzania iliuridhia Mwaka 2003. Aidha, Tanzania ilisaini Itifaki hii tarehe 27 Januari, 2005 ikiwa ni moja kati ya Nchi 45 zilizotia saini.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilibaini kuwa Ibara ya 2 ya Itifaki hii inarejea Ibara ya 3(d) ya Itifaki ya Kuanzisha Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika ya Mwaka 2002 *(Protocol Relating to the Establishment of the Peace and security Council of the Africa Union, 2002)* ambayo inazielekeza nchi kushirikiana katika kuendeleza mapambano dhigi ya ugaidi.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii, katika kuendeleza vita dhidi ya ugaidi kwa mujibu wa Itifaki na Mikataba ambayo Tanzania imekwisha saini na kuridhia, Bunge letu lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya Mwaka 2002 na kutungiwa Kanuni za kuzuia Ugaidi za Mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilipitia kwa kina vipengele vya Itifaki hiyo ili kubaini maudhui mahsusi ya Itifaki hiyo. Lengo ilikuwa ni kuelewa maudhui hayo na kuoanisha na mazingira ya Tanzania na hivyo kuweza kulishauri Bunge lako ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Maudhui ya ujumla ya Itifaki hiyo ni kuendeleza utangamano na ushirikiano wa Nchi Wanachama katika kuzuia matukio na vitendo vya kigaidi na hivyo kuendelea kudumisha Amani na usalama katika Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Aidha, kupitia Itifaki hii nchi wanachama ikiwemo Tanzania zitawajibika:-

i) Kuchukua hatua za lazima kulinda haki za msingi za binadamu dhidi ya vitendo vya kigaidi;

ii) Kuzuia uingiaji na utoaji wa mafunzo kwa vikundi vya ugaidi katika nchi husika;

iii) Kuainisha, kutambua na kuzuia au kukamata fedha na mali zilizotumika au zilizopangwa kutumika kwa ajili ya vitendo vya kigaidi na kuweka utaratibu wa kutumia fedha hizo kuwafidia waathirika wa vitendo vya kigaidi au familia zao; na

iv) Kuanzisha vituo vya kitaifa kwa ajili ya kubadilishana na kupeana taarifa za makundi ya kigaidi kwa wakati na shughuli za kigaidi katika ngazi za Kikanda, Kibara na Kimataifa.

Aidha, kamati ilibaini kuwa kupitia Itifaki hii Nchi wanachama ikiwemo Tanzania, zitaweza kupata taarifa na takwimu sahihi za wahusika wa vitendo vya kigaidi ndani na nje ya nchi. Pia, itawezesha nchi kubadilishana wahalifu wa kigaidi kupitia Makubaliano au Mikataba Maalum.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia maudhui ya Itifaki hiyo, Kamati ilijiridhisha kuwa Itifaki hii ina tija kwa nchi yetu ambayo si kisiwa kwa kuwa tumekuwa na matishio ya viashiria vya vitendo vya ugaidi ndani ya nchi. Mathalan, matishio ya viashiria vya ugaidi vimetokea katika mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Arusha, Tanga, Mwanza, Geita na Pwani. Vitendo hivi vinachangiwa na baadhi ya Wafuasi wa vikundi vya Kigaidi nje ya nchi kuvuka mipaka na kuingia nchini kwa lengo la kuendeleza vitendo hivyo vya kihalifu ikiwa ni pamoja na kueneza itikadi za msimamo mkali zinazopelekea watu kujiunga na makundi ya kigaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilijiridhisha kuhusu Nchi ambazo zimekwisha ridhia Itifaki hii ambapo Nchi 21 zimefanya hivyo. Kwa Afrika Mashariki Nchi za Burundi na Rwanda pekee ndiyo zimekwisha ridhia kati ya Nchi saba zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 3.1 Faida za kuridhia Itifaki

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya uchambuzi wa kina wa vifungu vya Itifaki hii kwa kuoanisha na matakwa ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 1999, Kamati imebaini kuwa zipo faida ambazo Tanzania itazipata kwa kuridhia Itifaki hii. Faida hizo ni pamoja na:-

i) Kuimarika kwa Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao;
ii) Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kutokana na kuwepo kwa amani na usalama nchini;
iii) Kuwezesha nchi yetu kushirikiana na nchi wanachama kulinda amani na usalama na kuhakikisha inalinda maisha na mali za watu;
iv) Kuwezesha kubadilishana wahalifu wa kigaidi kupitia makubaliano au mikataba maalum;
v) Kuwa na utaratibu wa kubadilishana taarifa miongoni mwa nchi wanachama kuhusu makundi na mienendo ya vitendo vya kigaidi na kuimarisha mtandao wa kupashana habari katika ngazi ya Taifa, Kikanda na Kimataifa;
vi) Kuweza kutumia kanzidata ya Kituo cha Afrika cha masuala ya ugaidi kilichopo Algiers, Algeria;
vii) Kutumia njia mbalimbali za usuluhushi endapo kutatokea mgogoro kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Itifaki;
viii) Kutumia Itifaki hii kama mwongozo wa kisheria katika kuanzisha makubaliano na nchi wanachama ambazo hazina utaratibu wa kubadilishana wahalifu wa kigaidi;
ix) Kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijinsia zinazohusu ugaidi kupitia ushirikiano na nchi wanachama;

x) Kuongeza ujuzi kwa wataalam wetu kupitia ubadilishanaji wa uzoefu na mafunzo na misaada a kiufundi; na

xi) Kuimarika kwa ushirikiano katika masuala ya urejeshwaji wa watuhumiwa wa Ugaidi.

xii)

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kujadili kwa kina hoja ya Serikali kuhusu Azimio la kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU) ya Kuzuia na kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004, Kamati inatoa maoni na Ushauri ufuatao:-

i) Bunge liridhie Itifaki hii kwa kuzingatia faida zitakazopatikana kutokana na uridhiwaji wa Itifaki hii;

ii) Kwa kuwa Sheria ya Kuzuia Ugaidi 2002 ni ya siku nyingi ikilinganishwa na matukio ya ugaidi ambayo yanaongezeka kila siku, Sheria hii ifanyiwe Marekebisho ili iendane na hali ya sasa. Aidha, Sheria hii iwe ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi na sio Kuzuia tu, Sheria iendane kama ambavyo Mikataba na Itifaki nyingi zinavyotaja *(Prevention and Combating of Terrorism;*

iii) Udhibiti wa uhalifu katika jamii ni vema ukaanzia katika ngazi ya familia, kaya, kitongoji na mtaa kwa kujengewa uelewa na umuhimu wa kutoa taarifa za uhalifu. Hivyo, serikali iimarishe mifumo ya utaoaji wa taarifa za kiharifu kuanzia ngazi ya familia;

iv) Kupitia Bunge lako Tukufu, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao hawajaridhia Itifaki hiyo washauriwe kufanya hivyo ili kuimarisha usalama wa Jumuiya hii; na

v) Kwa kuwa ukuaji wa uchumi unategemea usalama katika nchi, Serikali iandae Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ambao utaainisha hatua ambazo Taifa litachukua katika kuzuia na kupambana na Ugaidi; ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu elimu kwa umma na umuhimu wa kutoa taarifa kuhusu mienendo yenye mashaka ya watu, mitaala kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari ihusuyo mapambano dhidi ya ugaidi, uzingatiaji wa mgawanyo sawa wa rasilimali katika jamii n.k.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kuleta Hoja hii kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na

Usalama ili iweze kuifanyia kazi, jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Hamad Yussuf Masauni (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Christopher Kadio pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano katika kipindi ambacho Kamati ilikuwa ikishughulikia Itifaki hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa weledi, uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wa kufanyia kazi Itifaki hii. Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge *(Hansard)* pamoja na taarifa yote hii inayowasilisha maoni ya Kamati. Majina ya Wajumbe hao ni:-

1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Janeth Mauris Masaburi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb- Mjumbe
16. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb- Mjumbe
17. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Ally Mohamed Kassinge, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, n*dc* kwa Uongozi thabiti uliofanikisha uchambuzi wa Itifaki huu na uratibu wa shughuli za Kamati. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman

Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald S. Magili na Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria Ndg. Pius Mboya.

Kipekee kabisa nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii; Ndg. Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono Azimio hili na naomba Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki hii kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Vita Rashid Kawawa, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
19 Septemba, 2022

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa maoni hayo ya Kamati kuhusu azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea sasa na mjadala wa jumla tutaanza na Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo wajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninapenda kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni Naibu wake na timu yake nzima ambao tumekutana kwenye Kamati kwa takriban wiki nzima kupitia Azimio hili la Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi za Afrika kuzuia na kupambana na ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekitti, lakini pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wajumbe wenzangu wa Kamati, kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti wetu Vita Kawawa, kwa utulivu na umakini wa hali ya juu katika kuhakikisha kwamba tunafikia siku hii ya leo kuwasilisha hili azimio humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye masuala mengi mbalimbali kimataifa, jambo la kupambana na ugaidi ni jambo ambalo sisi kama Taifa na kama nchi ambayo hatuishi katika kisiwa tunapaswa kushirikiana katika kukabiliana na uhalifu mbalimbali ukiwemo vitendo hivi vya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa na kwa jinsi ambavyo vitendo vya ugaidi vyenyewe jinsi vilivyo; kwanza mpambano wa kigaidi si kama vita ya

kawaida ambayo pengine nchi A inaweza ikawa inapambana na nchi B, au kikundi cha mataifa kadhaa kikawa kinapambana na kikundi cha mataifa kadhaa, kwamba kitu ambacho kinaonekana. Tatizo la ugaidi ni vita ambayo adui kwanza humuoni na wala hujui yuko wapi na wala hujui anaishi wapi. Kwa hiyo, kwa ugumu huo maana yake ni muhimu sana kufanya jambo hili ili kukabiliana nalo katika namna ya kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa tumekuwa tukishiriki katika shughuli za ulinzi wa amani chini ya uratibu wa Umoja wa Mataifa na wakati mwingine chini ya utaratibu wa Jumuiya zetu za kikanda kama vile *SADC*. Kwa hiyo hata katika jambo hili ni muhimu sana kuhakikisha kwamba tunaendeleza utamaduni wetu wa kushirikiana na wengine duniani na kikanda katika muktadha mzima wa kuhakikisha kwamba tunakabiliana ipasavyo si tu na vitendo lakini ikibidi hata na viashiria vya masuala ya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mbalimbali chini ya utaratibu wa Umoja wa Mataifa au Umoja wa Kikanda kama nilivyosema tumeshiriki katika masuala ya ulinzi wa amani, ama katika eneo letu hili la maziwa yetu makuu ama hata katika nchi mbalimbali kama huko Lebanon nchi za Afrika za Kati, kote huko kuna majeshi yetu ambayo yanashiriki katika ulinzi wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi zote ni taratibu ambazo tunaziweka kimataifa ili kukabiliana na matukio au na vitendo mbalimbali ambavyo vinaweza vikahatarisha usalama si wa nchi yetu tu bali usalama wa eneo la kikanda na usalama wa dunia katika ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuridhia azimio hili la Bunge na Itifaki hii, sisi sasa pia tunaweza tukanufaika. Kama nilivyosema, suala lenyewe hili ni gumu kwa sababu napambana na adui ambaye kwanza umuoni na hujui yuko wapi. Kwa hiyo miongoni mwa faida ambazo tutanufaika nazo ni pamoja na ku-*share* taarifa. Kwa mfano tunacho hiki kituo cha kanzidata ambacho kipo pale Algeria, maana yake tukiwa sehemu ya hii Itifaki, sehemu ya hili azimio kuna taarifa sisi kama taifa tunaweza tukapewa ambazo tukazitumia katika kuhakikisha kwamba tunakabiliana si tu na vitendo lakini hata na viashiria vya ugaidi

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, kwa wanasheria wanaweza wakanisaidia; katika sheria, hasa sheria za kimataifa, kuna kitu kinaitwa *extradition* ambapo ni makubaliano baina ya nchi na nchi kubadilishana wafungwa. Lakini kupitia suala hili na azimio hili bado tunaweza kubadilishana wahalifu, tukawa na utaratibu maalum ambao unaweza kutuwezesha sisi kama taifa kubadilishana na wahalifu ambao kwa namna moja ama nyingine

wanashiriki katika vitendo au kwa namna moja au nyingine kuna viashiria kutokana na watu wao na masuala ya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia taifa letu tumekuwa tukifanya juhudi kubwa za kujenga uchumi wa nchi yetu, tunajenga miundombinu kama vile viwanja vya ndege; na kwa mfano sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa SGR. Hii ni miundombinu ambayo kwa namna moja au nyingine inasaidia katika kuvutia wawekezaji, inasaidia katika katika kuhakikisha kwamba tunapanua shughuli zetu za kiuchumi na kukuza biashara baina yetu na mataifa mengine, pia na baina yetu na majirani. Sasa, ili uweze kuwavutia wawekezaji, pamoja na miundombinu hii kama ya ujenzi wa barababara, kama nilivyosema ujenzi wa SGR, miundombinu ya nishati kama vile bwawa la umeme; lakini pia mwekezaji ili aje anataka awe na uhakika na usalama katika ile nchi au taifa analoenda kujiwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa moja wapo ya mambo ambayo ni muhimu kama taifa ni pamoja na kuhakikisha tuishi kama kisiwa, tunashiriki katika itifaki hizi ambazo ni za kimataifa au taratibu mbalimbali za kikanda. Kwa hiyo wanaangalia katika *list* na kuona kwamba hawa kumbe ni washirki katika jumuiya ya kimataifa na ni washiriki katika kikanda kuhakikisha kwamba kama taifa lao wanakuwa salama. Si wao tu lakini pia na majirani zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la utalii, kama nilivyosema tunaendelea na ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege. Kama sisi kule Iringa tunaendelea na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa. Pia hivi karibuni tutaanza ujenzi wa barabara kutoka Iringa kwenda *Ruaha National Park*. Hivi vyote kwa namna moja au nyingine vitavutia watalii, pamoja na kutumia fursa ya kutangaza ile filamu ya *Royal Tour* ambayo inavutia watalii. Sasa, ili nao, watalii, waweze kuja katika nchi yetu yapo mambo ambayo ni ya msingi ambayo wanatazama. Wanaangalia, je, Tanzania kama Taifa inashirikiana kimataifa kwa kiwango gani na kikanda kwa kiwango gani katika kuhakikisha kwamba inakuwa tu si yenyewe salama lakini salama na watu na majirani wanaotuzunguka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mtu anapoangalia katika *check list* anaona kama taifa tumeridhia azimio kama hili, kama taifa tunashirikiana na jumuiya za kimataifa katika kuhakikisha usalama wa taifa letu na majirani kwa hiyo inampa yule mtu *confidence* ya kuja kutembelea kama mtalii, lakini pia nakuja Tanzania kama mwekezaji. Kwa hiyo, itoshe kusema kwamba, jambo hili ni muhimu na limeletwa wakati ambao ni sahihi, na kama kamati ambavyo imeshauri, na ile sheria yetu ya kukabiliana na ugaidi pia tuifanyie mabadiliko ili iweze kuendana na suala hili kama ambavyo tumesema iwe *combat and abrogation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato David Chumi. Tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi. Mimi nitajikita kwenye kueleza faida ambazo kama nchi tutazipata endapo tutaridhia itifaki hii ya Umoja wa Nchi huru za Afrika ya Kupambana na Kuzuia Ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugaidi kutokana na *nature* yake ulivyo ni vigumu sana kwa nchi moja peke yake kupambana nao. Ugaidi ni tukio ambalo ni *organized crime* na mara nyingi ni *cross border.* Ni tukio ambalo wanaoshiriki kulifanya wanakuwa ni watu wana mpango mkubwa na ambao unavuka mipaka ya nchi. Sasa nchi moja bila kushirikiana na wenzako ni vigumu sana na *almost impossible,* haiwezekani kabisa kupambana na ugaidi kwa kuendesha mapambano hayo peke yako tu kama nchi moja kama vile uko kisiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida kubwa ya kuridhia mkataba huu, itifaki hii; na mimi niwaombe sana waheshimiwa Wabunge wenzangu turidhie itifaki hii kwa sababu faida kubwa ni kwamba itaiwezesha nchi yetu ya Tanzania kushirikiana na nchi nyingine kuweza kupambana na huu ugaidi ambao nimesema kwamba ni *organized crime,* na *nature* yake ni matukio ambayo yanavuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gaidi anaweza akafanya ugaidi nchini kwako lakini mipango ya kutekeleza ugaidi huo ameifanyia nje ya nchi yako, na fedha za kutekeleza ugaidi huo zimetoka nje ya nchi yako. Kwa hiyo, kama hushirikiani na wenzako, na nchi nyingine ni vigumu sana na hutaweza kupambana na huo ugaidi. Na kuridhia kwa itifaki hii kutatuwezesha Tanzania kama nchi kushirikiana na nchi nyingine ambazo nazo zimeridhia ili kuweza kupambana na huo ugaidi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu Tanzania tulisaini Itifaki hii mwaka 2004 lakini haikuwa-*enforced* mpaka pale ambapo angalau nchi 15 ziliweza kuridhia, na ambayo ilikuwa ni mwaka 2014. Kwa hiyo utaona kwamba tangu *instrument* hii imekuwa-*enforced,* kuanzia mwaka 2014 mpaka leo ni kama miaka minane. Sasa, ukiangalia hali ilivyo sasa hivi kama nchi yetu tuna umuhimu sana wa

kushirikiana na wenzetu ili kupambana na kuzuia ugaidi. Hii ni kwa sababu wote tunafahamu kwamba nchi yetu sasa hivi kwa namna inavyokwenda kuna fedha nyingi sana na uwekezaji zinakuja. amezungumza hapa Mheshimiwa Chumi muda uliopita; kwamba kuna *flow* ya fedha nyingi za uwekezaji zinakuja nchini kwetu kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kimaendeleo na kiuchumi. Sasa, ili kuwapa *confidence* hao wawekezaji ambao wanaleta fedha zao kuja kuwekeza nchini kwetu ni lazima wawe na uhakika ya kwamba uwekezaji wao hautaathirika na vitendo vya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na njia moja ya wao kuwa na uhakika ni sisi kuridhia Itifaki hii ili tuwemo kwenye orodha ya nchi ambazo zinashirikiana kupambana na ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya faida za kuridhia mkataba huu zimeelezwa. Kwa mfano Barani Afrika kuna kituo ambacho ni kimoja tu kipo Algiers - Algeria ambacho ndicho kinachotunza taarifa za magaidi wote, mienendo ya magaidi, magaidi ni kina nani, wana mipango gani, taarifa zote zinatunzwa na kituo cha kanzidata ambacho kipo Algiers – Algeria. Sasa ili uweze ku-*access* taarifa hizo ni lazima uwe umeridhia mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi Wabunge tukiridhia mkataba huo maana yake tunaipa nchi yetu uwezo wa ku-*access* hizo *data* za magaidi, jambo ambalo litatusaidia sana kupambana na huo ugaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuridhia Itifaki hii kuna faida nyingi na hakuna hasara yoyote. Kwasababu kimsingi kama nchi tulishasaini hii Itifaki mwaka 2004. Kwa hiyo, *issue* ya kusiani haipo tena, sasa hivi ni *issue* ya kuridhia. Kwa kusaini maana yake ni kwamba wakuu wa nchi wali-*approve,* na ndiyo maana nchi kama Tanzania tukasaini. Kwa hiyo, sasa kinachotakiwa ili uweze kunufaika na faida zinazopatikana na Itifaki hii ni lazima uridhie. Kwa hiyo, tunachofanya sasa ni kuridhia tu lakini kusaini tulishasaini. Na tunaridhia ili tuweze ku-*access* hizo faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa mojawapo ya faida ni kubadilishana uzoefu na utaalam. Hizi nchi tunapishana uwezo wa kukabiliana na magaidi. Kuna nchi nyingine inakuwa na uwezo zaidi na inakuwa na *best practice* zaidi. Kwa hiyo, ukiridhia Itifaki hii maana yake ni kwamba unakuwa kwenye fursa ya kuweza ku-*share best practice* na nchi nyingine ambazo zina uwezo pengine zaidi yetu wa kupambana na magaidi. Kwa hiyo, hakuna haja yoyote ya kutoridhia kwa sababu tutakuwa tunajinyima fursa na faida nyingi ambazo zipo kwenye kuridhia kwa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu turidhie Itifaki hii ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Magaidi kwa sababu ina faida nyingi na haina hasara yoyote kwa nchi yetu, ili tuweze kujenga *confidence* kwa wawekezaji ambao sasa hivi kwa jitihada kubwa zinazofanywa na Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan, fedha nyingi zinakuja, kwa hiyo, ni lazima turidhie Itifaki hii ili wawekezaji wetu wawe na *confidence,* wawe na amani kwamba mitaji yao haitaathirika na shughuli na *operation* za kigaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge turidhie Itifaki hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi. Tunaendelea na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, wajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia na mimi fursa niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ambayo ipo mbele yetu. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kuwa uwasilishaji mzuri na pia hata Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Kawawa, naye amewasilisha vizuri na kimsingi taarifa hiyo imesheheni na mawazo yaliyopo kwenye taarifa ile kwakweli hata sisi kama Kamati tuliyajadili na tumeyaafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasimama hapa kutoa mchango wa ziada kuhusu hoja hii ya Azimio la kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Tatizo la Ugaidi Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo mimi nataka kulisema, la kwanza kabisa ni umuhimu wa maisha, umuhimu wa uhai ambao Mwenyezi Mungu ametuzawadia. Hatupaswi kabisa ku-*compromise* na uhai ambao ni zawadi pekee tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Sasa tunapoona mtu anacheza au anafanya utani au anachezea maisha ya mwanadamu asiyekuwa na hatia hakuna mtu hata mmoja atakayefurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Azimio hili ama Itifaki hii lengo lake ni kwenda kuhakikisha linalinda uhai wa mwanadamu. Na hasa sisi watanzania ambao tumekuwa ni nchi ya amani kwa kipindi kirefu, kisiwa cha amani, sasa yanapokuja matukio kama haya ya ugaidi yanaondoa kabisa ile heshima ya uhali ambayo Mwenyezi Mungu amempatia mwanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niwaombe Wabunge wenzangu waunge mkono hoja hii, waunge mkono Itifaki hii iweze kuridhiwa ili

sasa nchi yetu iweze kuhakikisha inanufaika na zile faida ambazo wenzangu wanazisema zinazotokana na Itifaki hii. Na kimsingi Itifaki hii imeshasainiwa na nchi nyingi. Nchi zipatazo 45 zimesaini ikiwemo Tanzania na nchi 21 zimeridhia. Kwa hiyo, sisi sasa tunaenda kuwa nchi zaidi ya 22 ambazo tayari zimesharidhia-*adopt* hii Itifaki kwa lengo la kuhakikisha tunabadilishana uzoefu, tunabadilishana taarifa kama ambavyo wenzangu wamesema katika kupambana na tatizo hili la ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tunavyofahamu panapokosekana amani hata shughuli za kibinadamu za kiuchumi hazifanyiki. Huwezi Kwenda kufanya kazi huku ukiwa na mashaka ukiwa huna uhakika na uzima na usalama wa mazingira uliyonayo. Ndiyo maana kuna watu hapa akiona mende ana mashaka hawezi tena hata kutoka, anakuwa na wasiwasi sasa hapa tunazungumzia suala la ugaidi adui ambaye humuoni, hujui ni wakati gani atatekeleza tukio. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuhakikishe tunaliridhia azimio hili ili tuweze kunufaika na faida zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kwenda kuridhia Itifaki hii itaisaidia nchi yetu kuhakikisha inachukua hatua za lazima za haki za msingi za binadamu dhidi ya vitendo hivi vya kigaidi. Vilevile itasaidia kuhakikisha nchi yetu inazuia uingiaji na utoaji wa mafunzo kwa vitendo vya kigaidi ama vikundi vya kigaidi vinavyojihusisha na haya masuala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo inaenda kuipa nchi yetu sasa nguvu, tena kwa kushirikiana na nchi zingine, kupambana na vikundi mbalimbali vinavyojihusisha na matendo ya kigaidi. Pia itasaidia kuainisha, kutambua na kuzuia ama kukamata fedha na mali zinazotumika katika masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugaidi, kama tunavyofahamu, mwenzangu mmoja amesema ni *organized crime*. Ni watu ambao wameungana. Kwa hiyo, inawezekana nchi ziko sehemu nyingine, Ulaya na kadhalika, zinakuja huku kwa njia zisizofaa, kuja kutumika kigaidi. Kwa hiyo, hii itifaki inakwenda kusaidia katika kuzuia fedha haramu za namna hiyo ambazo zinakuja kuhatarisha maisha yetu huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kusisitiza na kuwaomba Wabunge wenzangu, tuone umuhimu wa itifaki hii na kuhakikisha tunaungana kwa pamoja, tunairidhia ili iende kusaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itasaidia kuanzisha pia vituo vya Kitaifa ndani ya nchi yetu kwa ajili ya kubadilishana na kupeana taarifa za makundi ya kigaidi kwa wakati na shughuli za kigaidi katika ngazi za kikanda na hata Kimataifa. Kwa hiyo, tufahamu kwamba inawezekana kuna taarifa zimepatikana nchi

fulani au eneo fulani, sisi hatuna, lakini taarifa hizo zinataka kuathiri nchi yetu, kwa hiyo, sasa tunakwenda kupata uhuru ule ama uwezekano rahisi wa kupata taarifa kutoka sehemu nyingine ambazo zingekuja kutuathiri sisi huku nchini mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili *in a nutshell* ukizungumzia faida mahususi za itifaki hii, kwanza ni kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kutokana na kuwepo kwa amani na usalama. Kama ambavyo tumesema kule mwanzo kwamba jambo la kwanza ni amani na usalama katika nchi yetu. Sasa panapokuwa na usalama, ndipo shughuli za kibiashara na za kiuchumi zitafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uwekezaji tunaoweza kupata kama nchi yetu ina viashiria vya ugaidi ambavyo tulishawahi kuona hata huko nyuma. Watalii hawawezi kuja. Kukishakuwa tu na taarifa zozote kuhusiana na masuala ya ugaidi, watalii hawawezi tena kuja. Kwa hiyo, hii sasa inakwenda kutuwekea uhakika wa utalii na hata wageni na wawekezaji wa sekta mbalimbali katika nchi yetu katika kuhakikisha tunaimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia ushirikiano, itaipa nchi yetu uwezo wa kushirikiana na nchi wanachama katika kulinda amani na usalama. Hii ndiyo ambayo tunasema inaenda kuhakikisha uhai ama kulinda mali za watu pamoja na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nalo ni la muhimu ni kuhakikisha tunakwenda kubadilishana utaalam na masuala ya misaada ya kiufundi. Sisi tuna *limitation,* kuna wenzetu wengine ambao wame-*advance,* kwa hiyo, tunaporidhia hili, ina maana tunaenda kushirikiana na wenzetu wengine ambao wame-*advance,* wana utaalam na pia ufundi uliopo ili tuweze kushirikiana, tuutumie katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa nasema hii inaenda kuisaidia nchi yetu; kama unavyofahamu, kumekuwa na taarifa nyingi kwamba kuna watu wanasema watuhumiwa wengi wa ugaidi wanakamatwa, wanakaa muda mrefu magerezani, wanashikiliwa, wanateswa. Kwa hiyo, hii pia inakwenda kutusaidia, na nchi inakwenda kupata namna ya ku-*deal* na zile kesi za watuhumiwa wa masuala ya ugaidi kwa urahisi. Badala ya kukaa muda mrefu magerezani, hii inakwenda kutusaidia pia katika kuhakikisha hatua zinachukuliwa. Pia hata kuwarudisha wale walioko nje, walioko Tanzania wa nchi nyingine waende kwenye nchi zao, Watanzania walioko nje warudishwe kwa ajili ya kufuata taratibu za kisheria ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuridhia itifaki hii kwa pamoja ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama na inaepukana na masuala haya ya kuishi kwa hofu na mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo. Nilimtaja Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, wajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ilipita toka mwaka 2004 na nchi yetu ilisaini, lakini leo, miaka 18 baadaye, inaletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhia. Ni hoja muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwaambie Wabunge wenzangu, kama nchi, tunakosea sana tunaposaini mikataba mbalimbali ya Kimataifa, lakini ukifika wakati wa kuridhia na kupitisha Bungeni mnaleta kwa kuchelewa. Mmekosea sana, miaka 18 ni mingi sana. Mheshimiwa Waziri, kwa kweli umelicheleweshа Taifa letu kuweza kusimamia nafasi hii ambayo leo tunataka tuifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nimesikia Wabunge wenzangu wakiwaomba Wabunge waweze kuipitisha na kuiridhia. Ilitakiwa tuiridhie miaka 18 iliyopita. Hivyo basi, ninaamini leo, sote kwa umoja wetu, tutaipitisha ili tuweze kuisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki hii ni ya muhimu, kama nilivyotangulia kusema, lakini nitaisema kwa upande wa pili. Sisi kama nchi tunapoenda kuiridhia, tunaomba tafadhali sana isimamie haki za binadamu. Kwa sababu itakapopitishwa, isichukue wale ambao ni watu wametuzidi kisiasa, wametuzidi kwa mambo mbalimbali ya kibinafsi wakati mwingine, kiongozi aliye madarakani au chama kilicho madarakani kikaamua kukandamiza watu kwa kupitia itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba itifaki hii itakapopitishwa, watu wafuatiliwe kiuhalali, wasimamiwe kama ni magaidi wafuatiliwe bila kuwabambikia. Kwa sababu tukiacha wazi watu wengi sana wasiokuwa na hatia wataweza kuhukumiwa, na baada ya miaka mitano, 10, 15, tunakuja kusema hawakuwa magaidi, tunawaachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hiyo hiyo kuna kipindi cha hapo nyuma watu wamefilisiwa mali zao, wamefungiwa akaunti zao za benki, wameshikiliwa pesa zao zisitumike mpaka uchunguzi uishe. Tunaomba itifaki hii ikasimamie haki za watu kama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, Ibara ya 18 ya Katiba inataka uhuru wa kujieleza, uhuru wa kutoa mawazo. Tunaomba itifaki hii isije ikawabana wale watu ambao wanatoa mawazo yao kwa ajili ya nchi yao, wakiwa wanatoa mawazo kwa ajili ya mambo mbalimbali yakiwemo ya kisiasa na ya kijamii, wasihukumiwe kama ni magaidi. Tunaomba ibara hii iwalinde na isimamie haki za hao watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume cha kufanya hayo, itifaki hii itaondoa amani na kuweka watu katika makundi, kwamba kuna watu wanaostahili kusema kitu fulani na kuna ambao hawastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hii itifaki pia iwashike wenzetu wa Jeshi la Polisi, waisome vizuri na kuiangalia. Kifungu cha tatu cha wajibu wa nchi washirika, kwa maana ya sisi ambao tunaingia itifaki hii, kipendele (a) kinasema hivi: "nchi mwanachama lazima ichukue hatua zote za kulinda haki za msingi za binadamu na kuhakikisha watu wake wanalindwa." Watu wasipigwe, watu wasiumizwe wakiitwa magaidi wakati bado haijachunguzwa kama kweli hao watu ni magaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba ndugu zetu Polisi, maana yake wao watakuwa karibu sana na sheria hii na ndio watekelezaji kwa asilimia kubwa. Wasimhukumu mtu, hata kumtoa kwenye magazeti kama ni gaidi wakati bado hajathibitika kuwa gaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia habari za haki na umoja wa Watanzania. Tunaomba sana, itifaki ni ya muhimu, na ni vizuri kama walivyosema waliopita, nchi yetu inaingia kwenye uchumi wa kati, na kama inaingia kwenye uchumi wa kati, tunahitaji kuwa na amani na ulinzi, hata wawekezaji wanavyokuja kuwekeza wanajua tunakwenda sehemu salama. Mwisho wa siku tusiitumie vibaya tukafanya vibaya, hasa inagusa wanasiasa kwa sababu wanasiasa watakapoguswa, siasa ni hisia. Unapomkamata kiongozi wa kisiasa au mtu ambaye ameshindwana na ninyi kwenye mambo ya kisiasa mkamsingizia mambo ya ugaidi, amani itatoweka, watu hawatasimamia shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba itifaki hii ipite. Nami nawaomba Wabunge wenzangu tuipitishe, lakini Serikali iliyopo madarakani ihakikishe itifaki

hii inakwenda kusimama kwa haki kwa magaidi wa kweli na wala siyo magaidi wa kubambikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda. Nilimtaja Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, wajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niwe sehemu ya wachangiaji katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naomba niseme kwamba amani tuliyonayo Watanzania ni mtaji, amani tuliyonayo ndiyo kivutio cha wawekezaji, na amani tuliyonayo ndiyo msalaba tulionao na tunatakiwa kuutunza kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Uhalifu na ugaidi ni vitu vinavyoendana. Tofauti yetu hapa ni maana ya neno ugaidi. Ila ugaidi ni uhalifu uliokithiri ambao unaweza kutoka nchi moja kwenda nyingine. Yuko mwenzetu amesema hapa kwamba vitendo vya kigaidi vinaweza vikapangwa katika nchi nyingine lakini vikatekelezwa katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini hapa? Ni kwamba amani tuliyonayo kama Watanzania haikuja kwa bahati mbaya. Amani tuliyonayo haikai hapa kwa bahati mbaya, ipo kwa sababu kama Taifa tumeamua; ipo kwa sababu Taifa linawekeza fedha nyingi kwa ajili ya kulinda amani ndani na nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kuendelea na ili tuweze ku-*maintain* amani tuliyonayo, sisi kama Watanzania, majirani zetu na dunia yetu, ugaidi ni jambo linalosomewa. Huwezi ukaibuka tu leo ukawa gaidi. Kuna vitendo vya ku-*recruit,* ku-*train* na ku-*equip.* Lazima uwezeshwe uwe gaidi, huwezi ukaamka leo ukasema mimi nataka kuwa gaidi, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo haya hayaji kwa bahati mbaya. Sisi kama Watanzania tuna mtihani mkubwa kwa sababu amani tuliyonayo wenzetu inawapa matatizo na wako katika kutujaribu kila siku, kwamba kwa nini Tanzania iendelee kubaki kuwa na amani? Kwa nini wawekezaji waende Tanzania? Kwa nini tusiharibu *image* ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ombi langu kwa Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba itifaki hii, pamoja na kuchelewa kwake, lakini sasa ni wakati mzuri kwa sababu tumeichakata kwa kipindi kirefu, tumeangalia *pay turn* ya matatizo. Maana yake, ugaidi, kama alivyosema mwenzangu, unaweza kupangwa eneo lingine lakini ukaja ukatekelezwa kwenye nchi nyingine. Sisi kama Watanzania kwa sababu Tanzania siyo kisiwa, na kwa sababu tunaweza kuondoa tatizo moja kulipeleka eneo lingine, Tanzania ni eneo ambalo kila mtu ametazama na angependa kutujaribu kuona kwamba kwa kweli tunataka tuvunje historia ya Tanzania kwamba ni eneo la amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenu; kwanza, turidhie itifaki hii kwa sababu Tanzania siyo kisiwa, Tanzania ni eneo ambalo tunaishi na wenzetu na walishafanya *ratification,* nasi kama sisi tunahitaji kuwa sehemu ya dunia. Kwa sababu matukio haya pamoja na kwamba yalitokea muda mrefu kwenye maeneo mengi, lakini bado yanaendelea kwenye nchi za wenzetu, nchi za jirani zinaendelea. Nasi tumekuwa tumo kwenye majaribio. Majaribio haya ni viashiria vya kwamba bado ugaidi unaendelea na sisi kama Taifa tunahitaji taaluma, nyenzo na kuendelea kuji-*equip* ili tuhakikishe kwamba tunaendelea kubaki kuwa salama. Kwa sababu wawekezaji kila siku wanatafuta wapi wataweka fedha zao ambapo pana amani? Bila ya hivyo tutaendelea kuwapoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo niwape mfano. Tanzania inasifika baada ya *Royal Tour. Royal Tour* hii haikuja kwa bahati mbaya, wala siyo bahati mbaya, ipo kwa sababu vyombo vyetu viko imara, havidharau taarifa na vinaendelea kutafuta taarifa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwetu ni kwamba tusidhani kwamba tumechelewa, hatujachelewa, lakini ni wakati muafaka ili sasa tuweze kuingia kama Taifa kwenye mataifa mengine tuweze kupata kila ambacho kinastahili kupatikana ili tuweze kufanya zoezi hili lifanyike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiyo, hatuingii eti kwa sababu tu tumeingia. Tumejiridhisha vya kutosha kama Kamati, tumejiridhisha kama Taifa kwamba sasa ni kipindi muafaka kwa sababu matukio yanayoonesha ni ishara na viashiria kwamba bado tunawindwa kama Tanzania, bado tunayo nafasi ya kuungana na wenzetu. Vile vile hatusubiri tatizo litokee. Ndiyo maana sheria zetu zinasema kwamba tuna-*prevent* kwanza halafu ndiyo runa-*combat.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenu ni kwamba turidhie itifaki hii ili tuweze kuendana na tuweze kutumia *facilities* zote zilizoko dunia nzima kuweza kupata taarifa na kuzitumia kwa ajili ya kushughuika na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiyo, wanaokuwa-*recruited* ni vijana wetu, watoto wetu wadogo ambao wanaghilibiwa ili kuweza kuingia wakioneshwa kwamba hapa kuja jambo haliko sawa, kwa hiyo tuingie. Kwa hiyo, naomba; mwenzangu amesema hapa, na Mheshimiwa Waziri amesema, kwamba mara nyingi hili linatakiwa lianze ulinzi kwenye nyumba zetu, familia zetu, mitaa yetu, ili kila mmoja aweze kufahamika tabia zake na nyendo zake, itusaidie kuendelea kulinda heshima yetu kama Taifa, itusaidie kutulinda sisi na kuhakikisha kwamba na wenzetu wanaendelea kuwa na amani na imani kwamba Tanzania bado ni nchi iliyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile na watoto wetu, kwa sababu hili siyo kwamba tumelizungumza kama Kamati kwamba hatuna ushahidi. Kama mtakumbuka miaka michache nyuma, watoto waliotoka Uingereza na Mataifa mengine, wamevutika tu na neno ugaidi, wamekuwa *recruited* wamekwenda kufunzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwamba ili tuweze kuwazuia watoto wetu wasiingie katika mkumbo huu wa kughilibiwa na wakadhani kwamba hiki ni kitendo cha fahari, siyo fahari. Ugaidi ni tendo la kudhalilisha utu wa mtu na sisi kama Bunge tunayo nafasi na wajibu wa kuhakikisha kwamba tunazuia vitendo hivi visifundishwe kwa watoto wetu kwa kuwa-*recruit* lakini kuwapeleka halafu wakaja wakatudhuru sisi au wakadhuru binadamu wengine wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana kwamba hili tulichukue, turidhie ili tuendelee kuwa Taifa lenye salama na amani ili tuendelee kubaki kama Tanzania ambayo tumeirithi na sisi tuwarithishe vizazi vyetu ikiwa bado ni Taifa lililo salama. Ninawaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema kwamba amani tuliyonayo ndiyo mtaji, amani tuliyonayo ndiyo fahari tuliyonayo ambayo dunia nzima inaihitaji na tungependa kama Kamati, kama Bunge, tuendelee kuwa Taifa lenye utulivu na kila mtu akiliheshimu akijua kwamba hapa ndipo eneo la kukimbilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuliko hayo, nimezungumza hapa nyuma kidogo kwamba *Royal Tour* haikuja kwa bahati mbaya. *Royal Tour* imetufungulia mambo mengi sana lakini moja kubwa zaidi ni kuongeza imani ya watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwape kisa kimoja. Watalii ni kama njiwa. Kama wapo wenzangu hapa waliowahi kufuga njiwa; njiwa kwa kawaida hata ukimwaga mchele anakuja mmoja mmoja, wa pili, wa tatu, wanakuwa wengi; lakini ukidondosha jiwe, wanaondoka wote kwa wakati mmoja. Kwa

hiyo, ombi langu, tusidhani kwamba jambo hili linawafurahisha wote. Hili linatufurahisha sisi kama Watanzania lakini tumepeleka au linaonekana ni tatizo kwa *competitors* wetu kwenye mambo ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana litusaidie kuhakikisha kwamba tunalinda *Royal Tour* yetu ya kwanza na ya pili na ya tatu itakayokuja kwa kuhakikisha kwamba tunaendeleza amani, na dunia iendelee kuamini kwamba bado Tanzania ni eneo salama, utalii uendelee na sisi tuweze kupata yale ambayo Taifa limejipangia ili kufikia malengo yake kwenye suala la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima sana, naomba niunge mkono hoja, lakini naomba turidhie kwa faida yetu kama Bunge, kama Taifa, kama *East Africa,* Afrika na jumuiya za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji. Nilimtaja Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa wajiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo Mezani inayohusu Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami nipongeze sana Wizara hii, nikianza na Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, Mheshimiwa *Eng.* Masauni, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara hii; na Naibu Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Sagini, ambao kimsingi sisi kama Kamati tumeshirikiana nao vizuri sana katika kuchakata itifaki hii mpaka leo inawasilishwa hapa Bungeni, nasi Wabunge tunapata nafasi ya kuchangia kwa lengo la kuomba Wabunge wenzetu waweze kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze na nimshukuru pia Mwenyekiti wangu wa Kamati, kaka yangu Mheshimiwa Vita Kawawa kwa namna ambavyo ametuwakilisha vizuri sisi Wanakamati wenzie katika kuwasilisha yale ambayo tulipokuwa kwenye Kamati ndiyo tumekubaliana kama Maoni ya Kamati ya kuwasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nitakuwa na mambo machache sana ya kuchangia ambayo yataongozwa na swali moja tu kwamba kwa nini sisi Tanzania kupitia Bunge lako hili tuweke Azimio hili la kuridhia itifaki hii. Jambo la kwanza *nature* ya ugaidi wenyewe. Kimsingi dhana

ya ugaidi si dhana ambayo inafanyika katika utaratibu wa kindani kwa maana *locally*, kinyume chake ni dhana ambayo inavuka Taifa moja mpaka Taifa lingine kwa maana ni dhana ya kimataifa. Kwa maana hiyo, kama ni jambo la kimataifa hatuwezi sisi Tanzania ambao tunajiita nchi iliyo kamili tukabaki wenyewe bila kushirikiana na nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, sisi Watanzania tukiridhia Itifaki hii, tutakuwa na fursa ya kuweza kushirikiana na nchi zingine za Afrika. Tukumbuke katika wasilisho ambalo Mheshimiwa Waziri amewasilisha hapa ni kwamba nchi 45 za Afrika zimesaini Mkataba huu ikiwemo Tanzania. Katika nchi hizo 45 ni nchi 21 ambazo zimeridhia na kwa maana hiyo sisi Watanzania tukiuungana au tukiridhia tutakuwa tumeungana na nchi zingine za Afrika 21 ikiwa ni pamoja na jirani zetu wa nchi kama za Rwanda, South Africa, Burundi, Lesotho, pamoja na nchi nyingine za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, kwa nini turidhie? Itakuwa imetupa nafasi au fursa ya kufanya marekebisho ya Sheria yetu iliyotungwa mwaka 2002, Sura Na. 19 ambayo tunasema ni Sheria ya Kuzuia Ugaidi na kwa maana hiyo tutakaporidhia Itifaki hii tutaweza kuwa na fursa ya kubadilisha Sheria yetu na kuwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ambapo sababu sheria zinatungwa hapa Bungeni, Wabunge tutakuwa na nafasi pana zaidi ya kutoa mawanda ya maelezo yetu maana wazoefu katika kuchangia sheria ambayo itakuwa na maslahi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa nini turidhie? Viashiria vya matukio ya kigaidi ni viashiria ambavyo katika nchi yetu tumeanza kuvisikiasikia kipindi kifupi kilichopita, lakini pia miaka kadhaa imepita nchi jirani siyo tu viashiria badala yake ni matukio ya kigaidi yameweza kutokea. Wote tunakumbua matukio ambayo yametokea Kenya miaka kadhaa iliyopita. Hivyo basi, hatuwezi kuwa salama kama jirani zetu au hata ndani ya nchi viashiria hivi vinatokea na sisi tuone kwamba tuko radhi hatuwezi kuridhia Itifaki hii, tukabaki salama hapana. Niombe sana Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono Itifaki hii ili nchi yetu iweze kusaini na kuridhia ili tuungane na nchi zingine za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph M. Mkundi, Mheshimiwa Nicholaus Ngassa na Mheshimiwa Kenneth Nollo wajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Itifaki hii

ambayo ni muhimu sana kama walivyotangulia kusema watangulizi. Nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati yetu mimi kama Mjumbe wa Kamati, kwa uwasilishaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii ni muhimu na hasa kwa kupata mustakabali mwema wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Taifa letu. Sisi Tanzania kama moja ya nchi ambazo siyo kisiwa tunachangamana, tunashirikiana katika nyanja mbalimbali na mataifa mengine yanayotuzunguka, hatuna namna yoyote tunayoweza kutafuta maendeleo ya Taifa letu kama kuna shida ya usalama kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka ya karibuni kumekuwa na shida ya usalama hasa kutokana na matukio ya kigaidi. Jambo ambalo limepelekea jumuiya mbalimbali kujipanga ili kukabiliana na matukio haya. Inapoletwa Itifaki hii leo katika Bunge lako Tukufu, niombe Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu tuweze kuliridhia Itifaki hii. Kwa sababu kupitia Itifaki hii, itafanya Taifa letu liweze kushirikiana na mataifa mengine kudhibiti lakini na kukabiliana na matukio ya kigaidi, lakini na kuzuia matukio ya namna hiyo vilevile. Leo tupo kwenye harakati za kujenga misingi imara ya kiuchumi ya Taifa letu. Hatuwezi kunufaika na misingi hii kama kutakuwa na shida ya usalama kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna pekee ni kushirikiana na wenzetu katika kukabiliana na matukio hayo. Tuweze kutambua ni *angle* zipi ambazo wahalifu kupitia ugaidi wanaweza kuzitumia na ni namna gani tunaweza tuka-*train* watu wetu kushirikiana na watu wengine katika kukabiliana na matukio haya. Yote haya hatuwezi kuyafanya sisi kaka Taifa tukiwa tumejitenga, ni lazima tushikamane, tushirikiane na mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ambavyo Mwenyekiti wa Kamati yetu amesoma taarifa yetu, tumechambua Itifaki hii, ni Itifaki muhimu na ya msingi sana Bunge letu kuweza kuridhia ili sasa kama mataifa mengine tuweze kushirikiana kudhibiti, lakini na kuhakikisha usalama wa watu wetu na mali zao unakuwepo ili sasa tuweze ku-*concentrate* kwenye kushughulikia mafanikio katika uchumi kwenye Taifa lakini na kwa mwananchi mmoja mmoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa uchache, niombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama ambavyo sisi taarifa yetu tumeiwasilisha kama Kamati, tuungane kwa pamoja kuridhia Itifaki hii ili sasa nchi yetu iwe nchi ya 22 kuridhia Itifaki hii, kuungana na mataifa mengine kushughulikia na kudhibiti matukio ya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi. Tunaendelea na Mheshimiwa Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo wajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Itifaki ya Mkataba ya Umoja Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi wa Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongea neno ugaidi, haraka haraka kichwani linakujia jambo linalohusiana na vifo, ukosefu wa udhibiti na amani, uharibifu wa majengo na miundombinu, kuzalisha vikundi vya uhalifu kwa maana ya *insurgency groups;* kuzalisha vikundi vya Itikadi kali kwa maana *Extremists groups;* lakini pia na umaskini katika nchi zetu. Sisi kama Taifa tumeamua kupitisha Itifaki hii ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi. Kwanza niipongeze Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoongozwa na Mheshimiwa Masauni, Naibu wake Mheshimiwa Sagini, lakini pia na Katibu Mkuu Ndugu Christopher Kadio; wameweza kufikisha Itifaki hii kwenye Bunge letu Tukufu na leo tunakwenda kuridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamechangia faida zitakazotokana na kupitishwa kwa Itifaki hii, nami kama Mbunge pia ningependa kuchangia machache ambayo naamini kama Taifa letu litanufaika kutokana na kupitishwa kwa itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza na la msingi kama Taifa wajibu wetu ni kuhakikisha ulinzi na usalama. Hiyo ndiyo dhamana kuu ya Taifa lakini pia ndiyo dhamana ambayo tumepewa sisi Chama cha Mapinduzi kupitia Serikali yetu hii ya Awamu ya Sita; kuhakikisha kwamba tuna ulinzi na usalama katika Taifa kwa maana ya *political stability*. Tutakaporidhia Itifaki hii, basi tutakuwa tunatengeneza mazingira mazuri ya kuhakikisha Taifa letu lipo salama na shughuli zote zinazofanya na wananchi zinaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo kama Taifa tutafaidika na Itifaki hii, ni kupata na kujengewa uwezo wa mafunzo na mbinu mpya za kupambana na udhibiti wa ugaidi. Kama ambavyo Itifaki inasema tutashirikiana na mataifa ya wenzetu na Jumuiya za Kikanda, tuna Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC* lakini pia Jumuiya mbalimbali za Kikanda ambazo tutashirikiana nao. Pia tutaendelea ku-*share experience* kwa maana ya uwezo kupitia vyuo vyetu mbalimbali vya mafunzo, sisi kaka Taifa tuna *NDC - Nation*

*Defense College* ambapo tumekuwa tukiona mataifa mengine yanaleta pale watu, Wakufunzi lakini pia na Maafisa mbalimbali wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa ajili ya ku-*share experience*. Kwa hiyo, kama Taifa tutajenga uwezo na tutapata mafunzo na mbinu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na la muhimu litakalotusaidia ni kuimarisha ushirikiano wa kikanda. Sisi Waafrika katika makuzi na malezi yetu tunaamini akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki, kwa maana ya kwamba tutakaposhirikiana kwenye changamoto mbalimbali za kukabiliana na hivi vikundi kama Boko Haramu, *Anti Balaka*, Ansar Dine, *Al-Qaida, Al-Shabab*, hivi vikundi mbalimbali vya kigaidi tutakaposhirikiana na mataifa mbalimbali, basi tutakuwa tunaimarisha ushirikiano wa kikanda, lakini pia inafanya tunakuwa wamoja na matatizo ya majirani zetu na sisi yanakuwa matatizo yetu. Atakapopata jambo Msumbiji, basi Tanzania utakwenda mbele, utakapopata jambo Tanzania, Malawi atakwenda mbele na hivyo hivyo ndivyo tunavyojenga ushirikiano wa Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne na la mshingi ambalo tunaweza kulipata kupitia Itifaki hii ni kuweza kutumia kanzidata ambayo ipo Algeria kama ambapo Waheshimiwa Wabunge wamesema. Katika kupambana na ugaidi nyenzo muhimu kuu ni mbili; kwanza ni taarifa na jambo la pili ni fedha. Sasa kwenye suala la taarifa tutapata *access* ya *data* kupitia itifaki hii tutakapoiridhia kama Taifa. Hii itatusaidia sana kuwa na taarifa, lakini pia ugaidi unashamiri sana kwa kupitia pia taarifa na fedha. Kwa hiyo, hivi vitu vinategemeana, lakini kama Taifa kwa kuwa tumepata *access* ya hii kanzidata maana yake tutakuwa tunapata taarifa mapema lakini pia tunaweza kujiimarisha na kudhibiti ugaidi katika Taifa letu lakini pia katika Jumuiya ya Kikanda zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano na la muhimu, ni kuimarisha kwa uchumi wa nchi, kuongeza uwekezaji na ustawi wa jamii. Katika mataifa ambayo yanakabiliwa sana na wimbi la ugaidi, ni vigumu sana kwa uchumi kuimarika lakini pia na wawekezaji wanakuwa na mashaka ya kuwekeza mitaji yao. Kwa hiyo, kama Taifa tunaishukuru Serikali kwa kuweza kufikia hatua hii katika hili jambo zito na la muhimu, tuendelee kuimarisha usalama wa Taifa letu na kuhakikisha tunavutia uwekezaji na hatimaye kukuza ustawi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa. Tunaendelea na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii kwa dhati niipongeze Serikali kwa kuja na Azimio la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Kupambana na Ugaidi. Zaidi jambo hili linatoka kwa pendekezo na muktadha kutoka Umoja wa Mataifa kwamba nchi katika Kanda mbalimbali na dunia kwa pamoja tuweze kushirikiana kupambana na ugaidi. Bahati mbaya, dhima na dhana hasa ya ugaidi bado inatofautiana kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Vilevile bado kuna ulegevu mkubwa wa Umoja wa Mataifa wenyewe kutoa *definition* kamili ya nini maana ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugaidi umekuwa unafadhiliwa na baadhi ya mataifa makubwa waziwazi na *UN* ipo. Ugaidi umekuwa kama unataka kuua mbwa mpe jina baya, baadhi ya nchi zimejaribu kutengeneza ugaidi kwenda kudhuru nchi zingine. Siwezi kuzitaja nchi hizo lakini ipo *sponsored terror groups* na jambo hili linatokana na mtofautiano wa kiitikadi kwamba huyu ni gaidi, kwa hiyo anaweza kuwa gaidi kwa mtizamo wa mwenzangu lakini kwangu vilevile asiwe gaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika historia wakati wa mapambano ya Kusini mwa Afrika, kikundi cha Nelson Mandela na Wapigania Uhuru wote wa South Africa waliitwa magaidi. Jambo hili bado linaendelea hata duniani, Mwalimu Nyerere alikwenda ziara Iraq mwaka 1979, wakati wanatoa ile inaitwa *International Communiqué* sasa maazimio ya pamoja na Iraq; Rais Sadam Hussein akataka waweke na kipengele kwamba kwa pamoja wamekubaliana kupinga uonevu unaofanyika kwa Wamarekani Weusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alikataa akasema *we don't subscribe to that conflict;* japo kuwa sisi ni *PAN Africanism.* Kwa hiyo na sisi tunapoingia katika muktadha huu wa kupambana na ugaidi lazima kuwa na maeneo tusi-*subscribe;* lazima tuseme sawa lakini hili bado haturidhii kama ule ni ugaidi. Tukienda hivyo, tutaondoa ile dhana ya sisi kutumiwa, kwa maana ya kwamba mataifa makubwa na mengine yanayotufadhili katika mambo mbalimbali yanaweza yakatumia mwanya huu sisi kuingizwa kwenye migogoro ambayo haituhusu na kwa sababu tumeingia katika Itifaki hii, basi tutaonekana kwamba na sisi tuweze kuwa pamoja katika migogoro ambayo wanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema kwa maana ya kanzidata ambayo ipo Algeria kwenye *security* na kwa maana ya ku-*share information* ni jambo la msingi; lakini siyo kila *information* utataka uitumie. Kwa hiyo, naiomba Serikali katika jambo hilo kwamba ni lazima tuseme kuna maeneo tunakubaliana kwamba huu ni ugaidi na kuna maeneo mengine lazima tukatae tuseme huu siyo ugaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kutaja baadhi ya nchi na baadhi ya vikundi, lakini jambo hili linaendelea. Ukienda nchi kama Qatar kuna vikundi vipo pale lakini nchi zingine wanasema wale ni magaidi; lakini wamewa-*host* wanakaa pale. Ukienda Palestine inachukuliwa ni magaidi, lakini kuna nchi hata sisi wenyewe tunasema Wapalestine siyo magaidi. Kwa hiyo, muktadha huu usitupeleke moja kwa moja katika Azimio hili, sasa katika *context* ya Afrika na sisi hata Kikanda bado kuna maeneo tunakubaliana hatukubaliani. Serikali zetu lazima tuchukue wajibu kwamba tusitumie mabavu ya Serikali kunyanyasa vikundi vingine na tukavipa nembo ya ugaidi. Jambo hili katika *SADC* na Afrika kwa ujumla ni lazima tuliangalie, kupitia hili Azimio tuwe na *model* nzuri ya kusema ugaidi ni nini na namna gani tuna-*combat* nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu hapa yalitokea pale Rufiji ilikuwa ni ugaidi, lakini tumeona Msumbiji imekuwa ni ugaidi, wenzetu wa West Africa wanasumbuliwa sasa na ugaidi nchi karibu tatu zote zile. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba lengo letu tuwe katika nyanja zaidi ya kiusalama badala ya kushabikia ugaidi hasa kwa maana ya *context* ya dunia ambapo bado hatujakubaliana gaidi ni nani katika mtazamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nchi zetu na Serikali zetu ni lazima ziangalie mipasuko katika jamii kwa kuwapelekea rasilimali, mgawanyo wa rasilimali uwe unakwenda sawasawa; moja ya maeneo yanayozalisha ugaidi ni baadhi ya jamii kutengwa, ni baadhi ya jamii kuona sasa hawafaidiki. Vilevile nchi zetu zina utajiri wa madini, baadhi ya maeneo ugawaji wa rasilimali haujakaa sawasawa; kwa hiyo, Tanzania kama kioo na kama kiranja wa ugawaji sawa wa rasilimali, ni lazima tuzikumbushe nchi zingine za Afrika ambazo tunaingia nazo katika Itifaki hii kwamba, lazima kuwe na usawa wa kugawanya rasilimali ili kuondoa minong'ono katika vikundi vingine katika jamii na hasa kuzalisha ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni lazima sote tukubaliane kwamba mitazamo ya kidini imetumika katika ugaidi na kwa bahati mbaya yapo maeneo ambayo wamepata *indoctrination* hasa katika watoto wadogo na baadaye kuingia katika *stage* kubwa ya ugaidi. Pamoja na hilo lazima na Tanzania iendelee kuwa mfano katika hizi nchi nyingine za Afrika kwamba sisi tumewezaje kukaa na dini mbalimbali, tumewezaje kuishi pamoja na tumewezaje kuvumiliana katika kuwa makabila zaidi ya 127. Kwa hiyo, tunavyoingia kwenye Itifaki hii tuna kazi ya kuwaonesha wenzetu, tuna kazi vilevile ya kutoa somo kwamba ni namna gani katika jamii nyingi kwa ujumla na namna gani una *in grace zile differences* ili uweze kuwa na jamii ambayo haina mikwaruzano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo kama nilivyosema pamoja na kuingia katika itifaki hii sisi tuwe kiranja katika kuonesha wenzetu ni namna gani wanaweza wakakumbatia zile tofauti zilizopo, tumefanya hivyo katika miaka mingi, tumekuwa wasuluhishi migogoro ya Maziwa Makuu. Kwa hiyo, kama nilivyosema tuna jukumu kubwa lakini kikubwa zaidi tusitumie ugaidi katika *context* ambayo baadhi wanazo tofauti zao za kisiasa na baadhi ya vikundi vinafadhiliwa na Serikali za nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa Bunge ni Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, baadaye upande wa Mawaziri Mheshimiwa Pindi Hazara Chana Waziri wa Maliasilli na Utalii akae tayari na baadaye Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani nae ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwa upande wa Wabunge. Awali ya yote ninawashukuru Wakuu wa nchi zetu za Afrika kwa sababu iliwapendeza miaka hiyo ya nyuma ya 2004 kuandaa Itifaki hii. Ni jambo la kimapinduzi na la kipekee kwa sababu tumezoea kuwa na Itifaki za Umoja wa Mataifa au Taasisi zake kubwa za Kimataifa, lakini tunapofikia sasa mahali pa kuanza kuwa na Itifaki ambazo zinatokana na Afrika kwa ajili ya Afrika ni jambo linalofurahisha sana kwamba *AU* sasa inarejea katika kazi yake ile ya msingi. Mwanzoni ilikuwa ni mambo ya ukombozi lakini baadaye ikaendelea kuwa sasa masuala ya uchumi, usalama na ustawi wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba huwezi ukaitaja *AU* au *OAU* bila kuitaja Tanzania. Mwalimu Nyerere pamoja na wenzake waliokuwepo enzi hizo ndio waliokuwa waanzilishi na mbegu ile ndiyo inayomea mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, kipekee kabisa kwa kweli leo tunaporidhia Itifaki hii tunapaswa kabisa kutambua, kupongeza na kushukuru juhudi za Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo ameendelea kufanya juhudi za kutufanya tubaki pale turudi kwenye nafasi yetu, katika Itifaki ya Afrika na ya Kimataifa na katika mambo ya Kidiplomasia ya Afrika na ya Kimataifa hasa katika maeneo yanayohusu maslahi ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine hiyo ni sehemu ya jibu kwamba kwa nini tunaridhia Itifaki hiyo leo, Itifaki ya mwaka 2004, hizi ni zama sasa za kutokuchelewesha mambo ya Kimataifa ni zama sasa ya kuyatekeleza, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais na kwa kuridhia Itifaki hii leo tunaunga mkono hizo juhudi zake ambazo dunia nzima imeshaziona tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri nikataja kidogo juu ya hii tarehe kwa nini tunaridhia leo tusiwe wanyonge sana kwamba ni kuanzia 2004. Ukienda Ibara ya 10 ya Itifaki hii utaona imeelekeza kwamba mpaka nchi 15 zitakapokuwa zimesaini na *ku-deposit* (zimeridhia) ndipo ile Itifaki itaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi hizi 15 zilifikiwa mwaka 2014 miaka 10 baada ya ile Itifaki. Kwa hiyo, leo hii tusiseme kwamba tunafanya kazi ya mwaka 2004 hapana, hata tungeifanya hivyo isingekuwa hatujafanya kazi yoyote bila nchi 15 ambazo zilifikiwa mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugaidi kama ambavyo wengi wamesema ni uhalifu wa Kimataifa na unaovuka mipaka, ni tofauti na uhalifu mwingine. Tunayo Sheria ile ya Kuzuia Ugaidi Sura ya 19 ambayo kwa kweli inatuwezesha zaidi kupambana na ugaidi wa ndani *(Domestic Terrorism)* lakini haitoshi tunapokwenda kwenye ugaidi wa Kimataifa, kwa sababu, ugaidi wa Kimataifa sasa hivi unaweza ukapigwa hapa na mtu aliyepo kilometa 10,000 kutoka hapo ulipo au mtu anaweza akapiga hapa lakini baada ya nusu saa ameshatoka nje ya nchi hii. Kwa hiyo, ni muhimu kuridhia Itifaki kama hizi ambazo zinapanua wigo wa kuweza kushughulika na jambo kama hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo Sheria nyingine inaitwa *Mutual Assistants in Criminal Matters Act Cap*. 254 ambayo inasaidia katika kuchukua ushahidi katika kupekua na kukamata vitu ambavyo vimepatikana katika upelelezi na katika kukamata watu wanaokimbia ambayo inatumika kwa nchi mbalimbali, lakini bado hata yenyewe hiyo inashughulika na makosa yote siyo kama hii ambayo ni maalum kwa ajili ya ugaidi. Kwa hiyo, pamoja na Sheria hiyo lakini bado tumeendelea kupata changamoto kwenye suala la ugaidi kutokana na upekee wake. Kwa hiyo, kutokana na upekee wake ni lazima tuingie kwenye Itifaki kama hii ambayo itatusaidia kupambana na hili jambo kwa kushirikiana na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugaidi hata usipotokea hapa Tanzania ukatokea nchi nyingine bado unaweza kutuathiri sisi. Kwa mfano, naamini kabisa magaidi walivyopiga pale *Westgate* Kenya siyo Wakenya peke yao ambao walidhurika na kufa ni watu wa Mataifa mbalimbali inawezekana hata Watanzania. Hata kule Chuo Kikuu - Garisa pia siyo Wakenya peke yao nakumbuka kabisa kwamba katika watu waliokamatwa kupanga na kutekeleza ile njama, sisemi kupatikana na hatia mimi nazungumzia kukamatwa kama walipatikana na hatia hiyo ni baadaye, lakini mmojawapo alikuwa ni kijana wa Kitanzania. Kwa hiyo, maafa haya yanakwenda kila mahali hata Septemba 11 kule Marekani iligusa watu wengi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la ugaidi pia linagusa haki ya kuishi *(right to life)* ambayo ndiyo Mama wa haki zote kwa hiyo, kwa kuridhia Itifaki hii pia tunatekeleza matakwa ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kulinda haki ya msingi ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache labda ninashauri tu mambo mawili. Jambo la kwanza kwenye utekelezaji wa Itifaki hii hasa kwa upande wa mambo ya *movement* ya *finances* (fedha) ni vizuri tukawa waangalifu sana, kuna watu wengine huwa wanatumia tusiwe Wakatoliki kuliko Papa mwenyewe. Tusije tukaitekeleza hii Sheria kwa ukali mpaka tukazuia vijana wetu ambao wanataka kuibukia katika biashara za Kimataifa sasa. Tuwe na uchunguzi wa kina kabla hatujachukua hatua kwenye haya mambo ya fedha kwa sababu yanaweza yakatumika pia kufifisha juhudi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge ninayetoka Jimbo la Mpakani ninazo taarifa kwenye baadhi ya maeneo ambapo sisi tumekuwa wakali mpaka kuzuia biashara kwa upande wetu lakini wenzetu kule wakalegeza wakafanya biashara. Kwa hiyo, tuwe makini kidogo kwenye hilo kwamba tusije tukajiumiza wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu elimu sahihi juu ya ugaidi ni kitu gani na gaidi ni nani ili tusije tukaingia kwenye mtego wa kushabihisha ugaidi na kabila fulani na Taifa fulani na dini Fulani, jambo ambalo ni la hatari sana. Ni vizuri tu tukajua kwamba ugaidi ni uhalifu wa Kimataifa ambao unalenga tu maeneo yenye udhaifu *either* kwa kukosekana kwa haki kwenye uchumi au kukosekana kwa haki kwenye siasa na mambo ya uongozi, basi wanapenyea hapo hapo na kuingiza mambo ya ugaidi lakini hauna msingi wowote katika kabila lolote, hauna msingi wowote katika dini yoyote wala katika katika Taifa lolote lile. Elimu ni muhimu sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza tu nirudi kuipongeza Serikali kwa kuleta Itifaki hii sasa hivi, pia Kamati kwa kweli mimi binafsi, kwa sababu sitoki kwenye Kamati husika *wameni-impress* sana kuanzia taarifa yao na Wajumbe wa Kamati walivyochangia, kwa kweli wameonesha umahiri mkubwa wa kuelewa Itifaki hii ambayo wameileta, wametufungulia hata sisi ambao siyo Wajumbe wa Kamati na hatujawahi kuchangia kwenye Kamati kupata ukereketwa wa kutaka kuchangia kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono na ninaomba Bunge lako Tukufu liunge mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Sasa tunaanza upande wa Mawaziri, ninamkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Maliasili

na Utalii Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, baadaye Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atajiandaa kwa dakika 10. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwanza kuunga mkono Itifaki hii ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ni mdau mkubwa sana katika masuala haya.  Ninampongeza sana kaka yangu Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri lakini pia niishukuru Serikali kwa kutuletea Itifaki hii. Itifaki hii haijachelewa imekuja wakati muafaka, kwa kawaida kabla ya kuridhia huwa tunakuwa na mambo mengi sana ya kuangalia na kujiridhisha kwa hiyo, niseme tu kwamba imekuja muda muafaka na muda muafaka ni sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumepata watalii wengi sana, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan Amiri Jeshi Mkuu kwa kutuongoza vyema na amani ndani ya nchi hadi sasa tunapata watalii wengi. Nimekuwa nikisema kwamba watalii hawa wanakuja Tanzania siyo tu kwa kuwa tupo kwenye ramani ya dunia lakini kabla ya watalii kufika wanaangalia vigezo vingi. Kuna suala la uongozi bora, siasa safi na *political stability* ni miongoni mwa vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi zingetamani sana kupata watalii lakini watalii kabla ya kwenda wakiona nchi labda ina vita, ina machafuko wanasema huko hatuwezi kuenda. Sisi tumeingia kwenye rekodi ya dunia kama kisiwa cha amani, tuko kama kisiwa cha amani kutokana na uongozi bora wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ndiyo maana hivi leo unakuta watalii wanaingia kupitia mipaka yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Iwe ni mipaka ya nchi kavu wengine wanatumia njia mbalimbali za ndege na kadhalika lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na uzinduzi wa ile *program* ya Tanzania *(The Royal Tour)* na sasa tutakwenda awamu ya pili ya uzinduzi wa *(The Hidden Tanzania)* tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Itifaki hii yako maeneo ya kubadilishana taarifa, yako maeneo ya mashirikiano imeeleza vizuri sana Itifaki hii. Inasema kwamba *we are determined to ensure Africa active participation, corporation and coordination with the international community in its determine efforts, combat and to eradicate* masuala ya ugaidi. Haya ni masuala muhimu sana na niombe Bunge hili turidhie kwa kauli moja kwamba, Itifaki hii ya kupambana na kuzuia ugaidi ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa dhamana pia ya kulinda na kuendeleza misitu, lazima tuwahakikishie Watanzania wasiopungua takribani Milioni 55 tunasubiri takwimu za sensa, kwamba misitu yetu iko salama. Katika Itifaki hii imesema tutaendelea kubadilishana taarifa. Iko misitu ambayo inafanana na kushirikiana katika nchi zetu za *SADC*. Kwa mfano kuna misitu inaitwa Miombo hii ni misitu ambayo iko maeneo yetu ya Nyanda za Juu Kusini na inakwenda hadi nchi za *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mengi sana ya misitu tunapakana na nchi mbalimbali, hasa misitu hii kama jinsi ambavyo misitu yetu ndani ya Jamhuri ya Muungano iko salama ni lazima tubadilishane taarifa, kwamba hii misitu ya nchi jirani na kwenyewe kuko salama au kuna changamoto? Kwa hiyo, Itifaki hii inapokuja itatusaidia kutoa mashirikiano kati ya nchi zetu, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi za *SADC* kuona kwamba maeneo yetu ya maliasili na utalii yapo salama. Kwa hiyo, Itifaki hii ni muhimu, kupitia Itifaki hii itatusaidia kwanza kukabiliana na masuala ya ugaidi, kukabiliana na masuala yote ya machafuko lakini kikubwa kama nilivyosema hapo awali ni suala zima la kubadilishana uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugaidi kwa kawaida unakuwa ni *planned and organized,* sasa tukiweza nchi za Afrika kuja pamoja kuelimishana, kukumbushana namna bora ya kudhibiti masuala haya ya ugaidi itatusaidia sana. Kwa hiyo, nimesimama hapa kuunga mkono hoja hii, kuunga mkono Itifaki hii na niombe kwamba Itifaki hii imekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa utalii unachangia takribani asilimia 17 ya Pato la Taifa. Utalii unatoa ajira takribani milioni 1.5 na fedha za nje takribani asilimia 25, nusu ya eneo letu la Jamhuri ya Muungano ni misitu. Maeneo haya ya misitu mazingira ya utalii, lazima tuwahakikishie umma na Jumuiya ya Kimataifa kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo salama karibuni katika masuala yote ya utalii. Iwe ni utalii katika fukwe, utalii katika hifadhi mbalimbali katika mapori yetu na Ikolojia zote kwamba Tanzania tuko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha jambo hilo hivi sasa tumekuwa na mikutano mingi sana na haya ni mazao mapya ya utalii, mwezi wa Oktoba tutakuwa na mkutano wa *United Nations World Tourism Organization,* huu ni mkutano ambao utaleta wadau wasiopungua 600. Miongoni mwa *checklist* ambazo wanakuwa nazo ni kujiridhisha kwamba huko tunakokwenda wako salama? Kwa hiyo, kwanza wameshajiridhisha tuko salama lakini Itifaki hii itakuwa ni moja ya silaha ya vitendea kazi ambavyo tutaweza kulinda na kuendeleza usalama wetu ambao tunao. Kwanza, kwa kuwaelekeza nchi

nyingine ni namna gani unaweza kufanya kudhibiti masuala haya ya uhalifu na wao wawe salama kama Tanzania tukitambulika kama ni kisiwa cha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Tanzania tumekuwa mfano wakati wa kupigania uhuru katika nchi za Kusini mwa Afrika, kupitia Baba wa Taifa Mheshimiwa Nyerere alikuwa akitoa maelekezo kwa nchi zote za Kusini na hapa tulikuwa tunaweka makambi ya usalama. Kwa hiyo, suala hili la ugaidi kukabiliana nalo tumekuwa tukilidhibiti tangu wakati wa uhuru Tanzania imekuwa ni *sample* ndani ya Afrika, Tanzania imekuwa ni mfano bora. Kwa hiyo, leo tunapopitisha Itifaki hii ni wakati muafaka na ninaomba nichukue nafasi hii kwa kweli kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana Waziri wa Maliasili na Utalii. Ninamkaribisha sasa Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Itifaki iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wangu *Engineer* Masauni mchana huu, lakini nianze pia kwa kuwashukuru katika vitu ambavyo vimetupa unafuu sana leo tunapojadili Itifaki hii karibu wasemaji wote wamekuwa-*positive* wameunga mkono hoja nasi kwa kweli tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tunaridhika na yote yaliyotolewa kwa maana ya kuunga mkono hoja yetu, zaidi na ushauri mbalimbali uliotolewa. Kuna maangalizo kadhaa yametolewa ningetamani kugusia machache kadri ya muda ulionipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamerejea manufaa, ambapo wazungumzaji karibu wote wamerejea manufaa kama yalivyoainishwa na mtoa hoja kwenye ukurasa wa 10, ukurasa wa Nane aya ya 10 ambapo amechambua hoja karibu 11 zinazosema manufaa ya kuunga mkono ama kuridhia Itifaki hii. Kwa hivyo, tunashukuru nimeona Mwenyekiti wa Kamati pia amerejea manufaa haya, kwa hiyo manufaa kwa kweli ni makubwa kwa sababu, tayari kama nchi tunayo Sheria ya Kuzuia Ugaidi lakini tulikuwa tumesimama nchi kama nchi, lakini kama wasemaji wengi walivyozungumza masuala ya ugaidi huvuka nchi moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania watakuwa wanakumbuka na Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mnakumbuka kwamba, hivi karibuni

kumekuwa na matukio yametokea karibu na mpaka wetu na nchi ya jirani kule *Mozambique*. Kwa hiyo, utaona uhalifu unafanyika Tanzania wanakimbilia kule, kwa sababu bila ushirikiano wahalifu wanaokimbia nchi jirani utawafanyaje? Kwa hiyo, ni lazima kuwa na Itifaki ya namna hii inasaidia fursa kama hizo za ushirikiano baina yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge wametukumbusha na mimi nalipokea, lakini tuwape tu *assurance* ni kwamba nchi yetu ipo makini, hatuwezi kwa sababu nchi moja au mtu mmoja kasema huyu hana sifa hizi mumuondoe Tanzania na sisi tukafuata na ndiyo maana kwa kulizingatia hilo tumechukua muda kujiridhisha na hadi tunapoleta Itifaki hii Bungeni tumejiridhisha kwamba tunachokwenda kufanya ni cha uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge miaka kadhaa iliyopita ziko nchi zilikumbana na changamoto za vikundi na kutaka *ku-blacklist* vikiwemo zile zinavyotoa huduma kwenye nchi yetu, lakini Serikali ya Tanzania haikukurupuka kufunga huduma zile tu kwa sababu nchi Fulani ilisema shule fulani, zahanati fulani kwa sababu ipo hivi ifungwe! Ni kwa sababu tulifanya uchunguzi wa kujiridhisha hakuna dalili zozote za kuonesha vitendo vya ugaidi kwenye eneo hili, kwa hilo nalo litaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi zilikumbana na changamoto za vikundi na kutaka ku-*blacklist* vikiwemo vile vinavyotoa huduma kwenye nchi yetu, lakini Serikali ya Tanzania haikukurupuka kufunga huduma zile kwa sababu tu nchi fulani ilisema shule fulani, zahanati fulani kwa sababu iko hivi ifungwe. Ni kwa sababu tulifanya uchunguzi tukajiridhisha hakuna dalili zozote za kuonesha vitendo vya ugaidi kwenye eneo hili. Kwa hiyo hilo nalo litaendelea na polisi wetu watajiepusha, kwa sababu hata Waziri alivyokuwa anaisoma alisema tutazingatia matakwa ya katiba, kuzingatia haki za binadamu ikiwemo kuepuka kubambikia watu wasiohusiana na makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hiyo inatukumbusha, mara kadhaa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, amevikumbusha vyombo vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutokubambikia watu kesi. Kwa hiyo hayo yanakwenda hadi hayo yatakayozungumzia masuala ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba na mimi niunge mkono hoja hii, kwamba Bunge kwa pamoja turidhie Itifaki hii ili tuweze kuungana na nchi nyingine 21 ambazo zimeweza kuridhia kwenye nchi zao ili tunufaike na uwepo wa Itifaki hii pamoja na wanachama wenzetu wa *OAU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Sasa nimkaribishe Mtoa hoja Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni Yussuf, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yetu ili aweze kuhitimisha hoja yake, karibu sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru na kuipongeza sana Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Vita Kawawa kwanza kwa jinsi ambavyo wanatupa ushirikiano na hata katika hoja iliyoko mezani. Mchango wao ulitusaidia sana, na leo hii hali kadhalika maoni na mapendekezo yao; nimuhakikishie Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kamati kwa ujumla kwamba yote ambayo wameyawasilisha tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikianza kuwashukuru waliochangia wote nianze na wewe Mwenyekiti kwa kuwasilisha mchango mzuri kwa niaba ya Kamati na wachangiaji wengine ambao walipata fursa ya kuchangia, ambao ni Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Seleman Zedi, Mheshimiwa Ighondo, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Zahor, Mheshimiwa Ally Kassinge, Mheshimiwa Nollo pamoja na Mheshimiwa Tadayo. Pia nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla maoni ya wachangiaji kwa asilimia kubwa sana au kwa asilimia zote niseme yanaonekana kuunga mkono Azimio hili ama Itifaki hii. Tunashukuru sana kwa kuunga mkono Azimio hili, lakini tunashukuru kwa kuweza kusaidia kuongezea kuelezea faida nyingi zaidi, ambazo kama taifa tutapata kwa kuridhia Itifaki hii, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kwa maelezo hayo na kwa maoni ya wachangiaji sitakuwa na mengi ya kuzungumza hapa leo kwa sababu mengi yaliyozungumzwa yanaenda sambamba na malengo na matarajio ya uwasilishwaji wa hoja yetu. Hata hivyo kuna mambo machache ambayo niliomba nitumie nafasi hii kuweza kuyapatia ufafanuzi kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo ningeomba nichangie ni hoja ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Mheshimiwa

Sophia Mwakagenda alihoji juu ya kwa nini tumechukua muda mwingi sana tangu Itifaki hii ilivyopitishwa na kusainiwa na kuweza kuwasilishwa leo hapa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, na nitajibu suala hili nikichanganya na hoja ya Mheshimiwa Nollo ambaye alitoa juu ya umuhimu wa kutofanya mambo kwa kufuata matakwa ya mataifa mengine ya nje, ambayo wakati mwingine hutumia changamoto ya ugaidi kwa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba taifa letu kama nchi tunafanya vitu kwa umakini mkubwa. Na kama ambavyo mnafahamu ilibidi tuangalie mambo mengi na tutafatakari kama taifa kabla ya kuwasilisha hapa Bungeni juu ya wakati gani ni mwafaka kuiwasilisha hatua hii. Na hiyo inadhihirisha juu ya uhuru wa taifa letu wa kuamua mambo yake yenyewe, kwamba hatufanyi mambo kwa kushinikiza. Pale ambapo tumeona sasa ni wakati ni muafaka kulingana na mazingira ya sasa hivi; na bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kwamba ni kweli taifa letu halijakumbana na changamoto za kigaidi, lakini tumeshuhudia viashiria mbalimbali vya kigaidi vikitokeza katika nchi hii katika nyakati kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata majirani zetu na wenyewe wamekumbana na matatizo ya kigaidi, na mfano mzuri ni hivi karibuni nilieleza hapa katika hotuba kwamba tulifanikiwa kuweza kuwapeleka watuhumiwa wawili wa kigaidi kutokana na tukio lililotokea Uganda. Hii inaashiria kwamba umuhimu wa Itifaki hii iko moja katika madhumuni yake makubwa ni kusaidia kubadilishana taarifa, kubadilishana uzoefu, kubadilishana mafunzo na ujuzi mbalimbali. Na pengine Itifaki hii itasaidia sana sasa kuweza kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sophia pia alizungumzia juu ya dhana nzima ya matumizi mabaya ya hoja hii ya ugaidi. Nataka nifafanue kwamba Tanzania tuna bahati kwa sababu tumekuwa ni nchi ambayo imejengeka katika misingi ya amani. Na kama ambavyo walizungumza, nadhani Mheshimiwa Zahor, kwamba vitu hivi havijaja kibahati mbaya. Kuna mambo mengi ambayo yamesaidia nchi yetu kuwa katika hali hii ya amani ambayo imekuwa ni mfano wa kuigwa Barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja ya sababu ambayo imechangia kufanya taifa hili liendelee kuwa na amani, ni kwamba misingi ya nchi yetu tangu imeanzishwa tumekuwa makini kudhibiti visingizio ambavyo vinatumika na baadhi ya nchi au baadhi watu katika nchi mbalimbali kufanya vitendo vya

kigaidi. Nchi yetu visingizio hivyo tumevidhibiti kwa kiwango kikubwa na jambo hilo limefanyika kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na vyombo vyetu vya usalama, lakini kubwa zaidi na waasisi wa taifa hili ambao walipata fursa ya kuongoza nchi hii katika miaka ya nyuma, vilevile pamoja na nchi hii kuweza kuwa katika mikono salama ya chama kilichopo madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi hiyo imesaidia sana kuvifanya visingizio vya kigaidi ambavyo vimekuwa vikitumika, aidha visingizio vinavyotokana na sababu za kikanda, visingizio vya kikabila, iwe visingizio vya kidini visipatikane katika nchi hii kutoka na uongozi dhabiti na imara ambao nimeeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka nilichangie, ni kwamba labda pengine Itifaki hii inaweza ikachangia matumizi mabaya yenye uhalifu wa kigaidi. Kwamba mtu anaweza tu akasingiziwa kwa sababu tu ya kutoa maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uhuru wa kutoa maoni upo kwenye Katiba, lakini kwenye Katiba hiyo hiyo uhuru huu umewekewa; maana katiba inasema bila kuathiri sheria za nchi; kwa hiyo uhuru huu umewekewa mipaka ya kikatiba. Uhuru wako unaishia pale uhuru wa mwingine unapoanzia. Na sheria za kudhibiti hizi ambazo zimeelezwa zipo sheria nyingi. Kwa mfano kuna Sheria ya Mtandao ambayo inatumika kuweza kudhibiti matumizi mabaya ya uhuru. kwa mfano leo hii huwezi ukasema una uhuru ukaanza kusambaza picha za ngono hovyo hovyo kwenye mitandao ya kijamii au ukazusha tu taarifa za uongo za kudhalilisha watu wengine, au ukazusha taarifa za kuchochea ubaguzi aidha wa kikabila, wa rangi au mwingineo na tukakaa tuseme tu kwamba huo ni uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe wasiwasi kwamba tunazo sheria ambazo zinadhibiti mipaka ya uhuru. Hatuwezi kutumia sheria ya ugaidi ama Itifaki hii kudhibiti uhuru wa watu, lakini uhuru wa watu utadhibitiwa pale ambapo utavuka mipaka ya kisheria kulingana na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu umuhimu wa sheria hii kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wameeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi waliochangia, wamezungumzia juu ya umuhimu wa sheria hii katika kuimarisha usalama katika nchi hii. Na usalama wa nchi hii ni jambo ambalo ni muhimu sana katika kusaidia kufanikisha hata kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kuna hoja zimezungumzwa kuhusu jinsi ambavyo taifa letu limepiga hatua kubwa sana hasa katika kipindi cha karibuni katika sekta ya utalii. Nimshukuru sana

Mheshimiwa Waziri wa Utalii amezungumzia vizuri hilo. Hatuwezi kuendelea kutumia fursa hiyo ya uchumi wa utalii kama amani katika nchi hii haijaendelea kutulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na matatizo ya kigaidi yamekuwa na athari kubwa sana katika kuteteresha amani ambayo inaathiri si tu utalii peke yake, yanaathiri utalii, uwekezaji, utabiri wa kimasoko *(market uncertainty),* lakini hata uingiaji wa fedha za kigeni nchini *(Foreign Direct Investment)*. unaathiri vilevile uwezo wa uchumi wa mtu mmoja mmoja, unaongeza umaskini. Kwa hiyo athari za kiuchumi zinazosababishwa na ukosefu wa usalama katika nchi ni nyingi, na ugaidi ni moja ya chanzo kibaya sana cha kuteteresha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mataifa mengi yakipata athari kubwa za muda mrefu, athari za kupoteza maisha, athari za kusababisha walemavu katika nchi husika, athari za matatizo ya kisaikolojia ambayo yanatokana na matatizo ya kigaidi. Pia athari za uharibifu wa mazingira na uharibifu wa miundombinu. Miji mingi imeharibika ambayo ilikuwa imejengeka vizuri tu kwa miaka mingi sana na kwa nguvu kubwa lakini leo hii imeharibika. Pia machafuko ya ndani na matatizo mengi sana ambayo yanasababishwa na matatizo ya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuunga mkono Azimio hili. Ni dhahiri kabisa Itifaki hii itakapopitishwa itasaidia sana kama taifa kuweza kujenga mahusiano na ushirikiano katika nchi yetu na mataifa mengine katika kukabiliana na athari za kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba sasa nimalizie kwa kutoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja

*(Hoja Ilitolewa Iamulie)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hoja imeungwa mkono sasa nitalihoji Bunge. Wanaokubali Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004 *(Protocal to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004)*. *(Makofi)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**(Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 *(Protocol to The OAU Convention on the Prevention of Terrorism, 2002)* Lilipitishwa na Bunge**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya sasa kukubali Wabunge wote Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilikubali na limeazimia na kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004 ambayo hiyo tumeipitisha sasa hivi.

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni Yussuf, Naibu wake Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Katibu Mkuu wao pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wamefanya mpaka leo hii wakaweza kuleta Itifaki hii na kuridhiwa na Bunge kama ni takwa la Katiba Ibara ya 63(3)(a).

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo baada ya kusema hayo nitumie fursa hii kuipongeza sana Kamati ambayo imeweza kuchambua na kupitia vizuri Itifaki hii, ambayo ni Kamati hii ya Mheshimiwa Vita Kawawa pamoja na timu yake kwa kuweza kuchambua vizuri Itifaki hii na hatimaye kuona manufaa ambayo nchi itaweza kupata na baadaye kuungana na Serikali na hivyo kuridhia. Hata hivyo pia niipongeze sana Serikali kwa kuleta Itifaki hii na leo kuridhiwa, lakini naamini kabisa kama Serikali itaona inafaa basi wanaweza kuleta muswada wa sheria ili kuweza kurekebisha ile Sheria ya Kuzuia Ugaidi, nafikiri ni Sura ya 19 ya Mwaka 2002 ili tuweze kubadilisha kama itakuwa haiendani na Itifaki hii.

Baada ya kusema hayo nitakuwa na tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwamba Jeshi la Polisi, Trafiki Makao Makuu Dar es Salaam limepanga kutoa elimu ya uendeshaji salama wa magari barabarani kwa madereva wa Waheshimiwa Wabunge, madereva wa Mawaziri, madereva wa idara zingine za Serikali walioko Bungeni na madereva wa Ofisi ya Bunge. Mafunzo hayo yatafanyika tarehe 20 Septemba, 2022 kwa madereva wa Waheshimiwa Wabunge na tarehe 21 Septemba, 2022 kwa madereva wa Mawaziri, idara nyingine za Serikali na madereva wa Ofisi ya Bunge. Mafunzo yatakuwa yakianza saa tatu hadi saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge, viongozi wa idara nyingine za Serikali mnaombwa kuwataarifu na kuwaruhusu madereva wahudhurie mafunzo hayo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zetu zimemalizika kwa muda huu basi niwatakie kila la heri Serikali katika utekelezaji wa Itifaki hii, lakini

niwatakie kila la heri Wabunge wote na mchana mwema. Naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 6:38 mchana Bunge Lilihairishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 20 Septemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*